Kikao cha Tatu – Tarehe 29 Septemba, 2017

(Kikao kilianza Saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Shehe Hamad Mattar) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Ofisi wa Makamu wa Pili wa Rais ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2016/2017, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, karibu sana.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa: Mhe. Mwenyekiti kwa ruhusa yako napenda kweka mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa Kuhusu Ripoti ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2016/2017, naomba kuwasilisha.

HOJA ZA SERIKALI

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Ripoti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2016/2017.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri karibu

Mhe. Waziri Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi aidha namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia asubuhi hii kutuwezesha na kutupa nguvu na afya za kuweza kuendelea na shughuli zetu kama tulivyojipangia.

Aidha Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe fursa hii kukushukuru wewe na viongozi wetu wote kwa kuliongoza vyema Baraza letu hili tukufu, aidha shukrani maalum zende kwa kamati yetu inayosimamia Ofisi zetu mbili hizi Kamati ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa iliongoza na Mhe. Mwenyekiti Omar Seif Abeid. *(Makofi)*

Aidha niwashukuru wajumbe wote wa Baraza hili Tukufu kwa namna ambavyo wanashirikiana pamoja na Serikali kuongoza shughuli za Taifa letu. Shukrani maalum zende kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza Mapinduzi kwa namna anavyoingoza nchi yetu kwa uadilifu

na busara na uvumilivu mkubwa wa kuongoza nchi hii Mwenyezi Mungu ampe baraka nyingi, mafanikio makubwa afya njema yeye na familia yake.

Aidha namishukuru Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa kumsaidia vyema Mhe. Rais katika utekelezaji wa majukumu mbali mbali na kuisimamia ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, yeye amekuwa dira katika kutongoza kutekeleza shughuli zetu. Baada ya maelezo haya Mhe. Mwenyekiti naomba sasa niendelee kwa kueleza yafuatayo.

Kama ilivyokuwa kwa kamati nyengine za kudumu za Baraza la Wawakilishi Kamati za Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa iliwasilisha ripoti ya shughuli inazozifanya kwa maka wa fedha 2016/2017 mbele ya Mkutano wa Tano wa Baraza Tisa la Wawakilishi la Zanzibar.

Katika ripoti hiyo Kamati ilitowa ushauri na maagizo mbali mbali ambayo yanapaswa kutekelezwa na ofisi zetu zinazosimamiwa na kamati hii, ambazo kwa awamu hii ni Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ripoti ya kamati hiyo ilibainisha changamoto mbali mbali zinazoikabili Idara na Taasisi zinazotembelewa na ilitowa ushauri na maagizo ambayo ofisi yetu imeyatekeleza kama inavyoonesha katika kipengele cha pili cha jadweli hili.

Mhe. Mwenyekiti, muundo wa taarif hili unahusisha agizo au ushauri uliotolewa na Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi la Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaaifa kwa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais na jinsi agizo au ushauri huu ulivyotekelezwa na ofisi yetu kupitia Idara au Taasisi inayohusika.

Mhe. Mwenyekiti, maagizo yalikuwa kama yafuatavyo:-

Tume ya Kitaifa ya Uratibu wa Udhibiti wa dawa za kulevya:

Agizo namba moja
Kamati imeitaka Serikali kupitia Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kuongeza bajeti kwa ajili ya Tume ya Kitaifa ya Utaratibu na Uthibiti wa Dawa za Kulevya katika bajeti ya mwaka 2017/2018 ili kuipa uwezo wa kifedha wa kukabiliana na janga hili la kitaifa.

Utekelezaji
Mhe. Mwenyekiti, Serikali imeongeza bajeti ya Tume ya Kitaifa ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya Zanzibar kutoka Shilingi milioni 439,900,000 kwa mwaka wa fedha 2016/2017 hadi shilingi milioni 598,900,000 kwa mwaka wa fedha 2017/2018 hili ni ongezeko la shilingi milioni 159,000,000 ambayo ni sawa na asilimia 36 ya bajeti ya mwaka 2016/2017.

Agizo namba mbili
Kamati imeitaka Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kuona haja ya kuifanyia marekebisho ya msingi Sheria ya Tume ya Kitaifa ya Uratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya ili kuipa uwezo na Mamlaka ya kutosha ya kusimamia wenyewe kesi zinazohusiana na dawa za kulevya.

Utekelezaji wa Agizo
Mhe. Mwenyekiti, katika suala la mapambano dhidi ya usambazaji na matumizi ya dawa za kulevya Serikali itandelea kuchukua hatua zote zinazostahiki kama zilivyoelekezwa katika Sheria zinazosimamia masuala ya dawa za kulevya, ikiwemo Sheria ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya ya Zanzibar namba 9 ya mwaka 2009 Sheria hii imekuwa ikifanyiwa marekebisho ya mara kwa mara ili iendane na mahitaji na wakati ulioko na ujao.

Aidha katika kutekeleza matakwa ya kifungu cha 49 cha sheria hiyo ambacho kinaipa uwezo tume kuandaa uratibu wa kuangamiza dawa za kulevya kutoka kwenye uhifadhi wa kisheria, Serikali imetunga kanuni mbili ikiwa moja ni viwango vidogo vya dawa za kulevya na moja ni ungamizaji wa dawa hizo.

Mhe. Mwenyekiti, kimsingi sheria iliopo hivi sasa ya udhibiti wa dawa za kulevya Zanzibar namba 9 ya mwaka 2009 bado ina kidhi haja ila kuna umuhumu mkubwa taasisi zinazohusika mapambano dhidi ya dawa ya kulevya likiwemo Jeshi la Polisi kuzidisha juhudi na kuwajibika ipasavyo kutekeleza majukumu yao kulingana na sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la kuipa uwezo mamlaka tume ili iweze kusimimia yenyewe kesi zinazohusiana na dawa za kulevya bado tume inaendelea kulitafakari kwa kina suala hilo kwa kuzingatia mafanikio na changamoto za mfumo au utaratibu huu ambao Mamlaka ya Kudhibiti Dawa za Kulevya ya Jamhuri ya Tanzania unautumia tangu 2016 kwa hivyo kwanza tunaka tujifunze uzoefu wa wenzetu ili tuweze kubadili hiyo sheria, tuweze kufahamu changamoto na mafanikio yao ndio itakayoweza sisi kutuwezesha kufanya maamuzi makubwa hayo.

Agizo namba tatu
Kamati imeshauri kuongezwa wa wigo wa utowaji wa elimu kuhusiana na dawa za kulevya na athari zake kwa kumia Taaasisi za Kijamii zaidi ikiwa ni pamoja na shule za msingi na madrasa za dini ambazo kuna uwekano mkubwa kila kijana kupitia ukizingati zaidi kwa jamiii ya kizanzibari ni jamii yenye malezi ya kidini.

Agizo hilo inakwenda sambamba na agizo namba nne ambalo limesema hivi:

Kamati imeshauri utolewaji wa elimu ya kutosha katika maeneo yalizunguka vitongoji na mitaa iliyoathirika kwa kiasi kikubwa na dawa za kulevya kipitia mkutano ya wazi makongamano na warsha mbali mbali ili kupunguza uwezekano wa janga hili kuongezeka kwa kasi katika maeneo mengine

Utekelezaji
Mhe. Mwenyekiti, kwa vile maagizo haya namba 3 na namba 4 yanafanana naomba kuomba kueleza utekelezaji wao kwa pamoja kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa Idara ya Tume za Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya ni Idara ya Kinga, Tiba, Elimu na Marekebisho ya Tabia. Moja ya majukumu ya Idara

hii ni kutowa elimu ni kutowa elimu ya kinga, tiba na marekebisho ya tabia kwa makundi mbali mbali na jamii kwa jumla.

Mhe. Mwenyekiti, katika kazi zake za kila siku Idara hiyo imekuwa ikifika katika sehemu za Kazi, Skuli, Taasisi za Elimu ya Juu na Mabaraza ya Vijana na katika mikusanyiko ya shughuli za kitaifa kama vile mwenge wa uhuru kwa ajili ya kutowa elimu juu ya athari zinazotokana na dawa za kulevya.

Tume pia imekuwa ikifanya mikitano na makongamano kwa viongozi wa dini, Masheha, wana jamii pamoja na watu mashuhuri katika jamii ili kuhakikisha kila sehemu inafika elimu ya juu ya athari za matumizi ya dawa za kulevya, hii ni pamoja na mikutano baina ya wazee na vijana walioathiriwa na matumizi ya dawa za kulevya ambayo inalenga kuhakikisha kuwa vijana wao wanaachana na dawa za kulevya na wanarudi kwenye familia zao na pia hawarudii tena na matumizi ya dawa za kulevya pamoja na kuwapa tiba za kisaikologia wanafanmilia pamoja na wazee na vijana hao.

Mhe. Mwenyekiti, tume kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa ya kupambana na uhalifu wa dawa za kulevya duniani UNODC inamilisha utaratibu wa kuwa kuwa na *program* maalum ya kuwakingza vijana na kuwaepusha na matumizi ya dawa ya kulevya. *Program* hiyo inayojulikana kama *Strong Family* pia inawashirikisha wahusika kutoka Wizara inayoshughulikia Elimu pamoja na Wizara inayoshughulika masuala ya vijana na watoto. Hata hivyo ushauri tunaupokea na tutaendelea na juhudu za kutowa elimu kwa umma juu ya athari za biashara na matumizi ya dawa za kulevya.

Agizo namba tano
Kamati imeshauri kuwepo kwa mikutano ya pamoja itakayofanyika mara kwa mara baina ya Watendaji wa Tume, Polisi, Waendesha Mashtaka, Mahakimu na Maofisa wa Tume ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ili kujadiliana na kujenga msimiamo wa pamoja wa kupambana na hatimaye kutokomeza kabisa janga hili ya kulevya linalondelea kupoteza nguvu kazi ya Taifa.

Mhe. Mwenyekiti, utekelezaji Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya katika utaratibu wake wa kazi huwa inatekeleza suala hili kila baada ya mwezi na limo katika bajeti yake ya kila mwaka.

Tume itaendesha mabaraza maalum ya majadiliano *secodize meeting* kuhusu kesi za dawa za kulevya ambazo hufanyika kila baada ya mwezi kwa lengo ya kujadili kesi za dawa za kulevya ili kujua changamoto zilizopo na namna ya kuzikabili.

Mhe. Mwenyekiti, tume pia hufatilia kesi zote zinazofunguliwa ili kujua mustakbali wake, uchunguzi wake na upeleleze wake hadi kufikia hatua kufungua jalada la mahakamani. Aidha tume hufuatilia matokeo ya kesi zake na kuyawasilisha Serikalini kama sheria inavyoelekeza kwa lengo la kuhakikisha kesi za dawa za kulevya zinapelekwa kwa kazi zaidi lakini pia kuhakikisha kwamba kesi hizi zinapata hatia na Jamuhuri hushinda kesi zake, na pale tume inapoona kuna upungufu ikiwemo taaluma tume hulichukuwa suala hilo na kulitafutia ufumbuzi wa kuwapatia wahusika elimu inayohusiana na kuendesha kesi za dawa kulevya.

Hatua hii tayari imeshaanza kutowa matunda kwani sasa kesi za dawa za kulevya ziko vizuri na Jamhuri zinashinda kesi zake, Serikali itaendeleza mashirikiano yaliopo kwa wahusika wote ili kufanikiwa katika mapambano dhidi ya biashara za madawa ya kulevya.

Agizo namba sita
Kamati imeshauri kuimarishwa kwa mazingira ya upekuwaji wa abiria na mzigo inayoingia na kutoka kupita bandari na viwanja wa ndege kwa Unguja na Pemba ili kuzuwiya uingizaji wa dawa hizo kwani kamati inahofia Zanzibar isije ikawa mingoni mwa njia inatumika sana kupitisha na kushafirisha dawa za kulevya kwenda katika mataifa mengine.

Utekelezaji
Mhe. Mwenyekiti, Tume imewailisha suala hili Serikalini na tayari Wizara inayohusika na bandari na viwanja vya ndege inalifanyika kazi. Aidha vyombo vyetu vya ulinzi na usala vinaendelea kulifanyika kazi kwa kina suala hilo sambamba na Serikali kuwa na mradi maalum wa Zanzibar Salama ambao pamoja na mambo mengine utatazingatia suala la namna ya kudhibiti ya usafirishaji wa dawa za kulevya nchini.

Agizo namba saba
kamati imeshauri kuwepo kwa mabango yanayoelezea adhabu na makosa yanayohusiana na dawa za kulevya katika maeneo yenye mkusanyiko wa watu na njia kuu za kuingia nchini kama vile bandari, uwanja wa ndege ili kuelezea na kutoa tahadhari kwa kujihusisha kwa namna yoyote katika dawa za kulevya ni uhalifu.

Utekelezaji
Mhe. Mwenyekiti, Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Uthibiti wa Dawa za Kulevya inaendelea kulifanyia kazi suala hili kwa kushirikiana na taasisi zinazohusika. Aidha tume iteendelea kutowa matangazo na elimu kuhusu athari na tahadhari juu ya biashara ya matumizi ya dawa za kulevya kupitia njia mbali mbali ikiwepo vipeperushi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa ni maeneo ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar.

Agizo namba moja
Kamati imeiagiza Serikali kupitia Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ihakikishe kwamba inakuwa na Ofisi ya Tume ya Uchanguzi katika kila Wilaya japo kwa majengo ya kukodi kwa kuanzia huku Serikali ikitafuta namna ya kujengza ofisi zake ili kila Wilaya iwe na Ofisi yake kwa lengo la kuwasongezea wananchi huduma zinazotolewa huduma zinazotolewa na Tume ya Uchaguzi karibu na maeneo yao.

Utekelezaji
Mhe. Mwenyekiti ni kweli Ofisi za Uchaguzi za Wilaya hazijawa ha majengo yao wenyewe isipokuwa Ofisi za Uchaguzi za Wilaya ya Mjini, Wilaya ya kati na Wilaya ya Kusini hatua za kuzungumza na mamlaka zinazohusika kuipatia tume maeneo ya kujenga Ofisi za kudumu za Wilaya zinaendelea, Serikali inachukuwa kila jitihada ili kuhakikisha kuwe lengo hili linafikiwa tunaishuru Kamati yetu kwa kutukumbushia suala hili.

Agizo namba mbili
Kamati imeshauri Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kupatiwa kiwanja kilichopo jirani na jengo la tume kinachomilikiwa na mtu binafsi kabla haijaanza ujenzi kwa hatua za awali lakini pia ili kuimarisha hali ya usalama zaidi kutafutwe namna ya kujenga uzio jengo la Ofisi ya Tume kwa ajili ya usalama wa watendaji na mali zake.

Utekelezaji
Mhe. Mwenyekiti, hatua za awali za kupima eneo la jengo linalotumiwa na Tume ofisi ya Wailaya ya Mjini pamoja na eneo la kiwanja kilicho wazi ni eneo la nyumba namba 3322 na nambari 2071 zimekamilika.

Kamisheni ya Ardhi imekamilisha hatua za ramani ya eneo hili ili iweze kuendelea hatua ya kutukabidhi hati za matumizi ya eneo hilo la Tume ya Uchaguzi. Katika suala hili Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein tayari alishatoa maelekezo ya kina juu ya matumizi ya eneo hilo la Tume ya Uchaguzi na ofisi yetu kwa kushirikiana na Wizara zinazohusika na masuala ya ardhi na majengo ya Serikali tutaendelea maelekezo hayo ili majengo hayo yawe chini ya Tume ya Uchaguzi.

Agizo namba tatu
Kamati imeshauri pia kutokana na ufinyu wa nafasi katika jengo linalotumika kwa sasa Serikali iwafikiria kuwapatia Tume jengo liliopo jirani na Ofisi za Tume ambalo halitumiki kwa sasa ili kupata eneo la kufunyia shughuli zake kwa ufanisi zaidi pamoja na kuhifadhi vifaa vyake vya uchanguzi.

Utekelezaji
Mhe. Mwenyekiti, jengo lililokusudiwa ni jengo linalomilikiwa na Shirika la Bandari, jengo Nam.2071 ambalo linahitaji matengenezo. Watendaji wa Idara ya Ujenzi walifika katika jengo hilo kufanya ukaguzi tarehe 20 Februari, 2017 kwa ajili ya kuandaa bajeti ya matengenezo na kuiwasilisha kwa Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi. Kuhusiana na suala la makabidhiano ya jengo hilo tayari serikali imeshatoa maelekezo na yanaendelea kufanyiwa kazi.

Agizo Nam.4. Kamati imeagiza kupigwa na mnada na kuuza magari machakavu yanayotumika na Tume ya Uchaguzi ambayo yatagharimu fedha nyingi kutengenezwa, na badala yake yanunuliwe magari mengine mapya japo machache kwa ajili ya kuendesha shughuli za tume ukizingatia umuhimu wa taasisi hii.

Utekelezaji.

Mhe. Mwenyekiti, ukaguzi juu ya uimara wa gari za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar umefanywa na Idara ya Karakana Kuu ya Serikali tarehe 20 Februari, 2017. Jumla ya gari 11 zilizopo Unguja na gari 6 zilizopo Pemba zimeruhusika na ukaguzi huu. Aidha, serikali imeipatia fedha Ofisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kwa ajili ya kutengeneza gari hizo. Hivi sasa ofisi inawasiliana na Idara ya Karakana Kuu ya Serikali kwa ajili ya utengenezaji wa gari hizo. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 serikali imetenga shilingi milioni 200,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa gari mpya ya tume.

Agizo Nam.5. Kamati imeshauri kufanyika kwa programu mbali mbali ambazo ni endelevu juu ya utoaji wa elimu kwa umma juu ya kazi, nafasi na hadhi ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar. Ili kufuta dhana mbaya zilizopo juu ya tume hiyo kuwa si tume huru inayojiendesha na yenye maamuzi yake.

Utekelezaji.

Mhe. Mwenyekiti, Tume ya Uchaguzi Zanzibar iliandaa na kurusha hewani vipindi 11 vya redio kuanzia mwezi wa Januari hadi Machi, 2017. Vipindi hivyo vinajuulikana kwa jina la kutoka Tume ya Uchaguzi Zanzibar, hurushwa hewani kupitia ZBC redio kila siku ya Jumapili saa 11:15 jioni. Madhumuni ya vipindi hivyo ni kuelezea mada zinazohusiana na uchaguzi ambapo vilianzia kwa kueleza dhana na historia ya uchaguzi Zanzibar kuanzia mwaka 1957 mpaka 2010. Na mada inayoendelea katika vipindi vinavyorikodiwa mwezi wa Machi ni kuhusu historia na uanzishaji wa daftari la kudumu la wapiga kura.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia mpango wa elimu ya wapiga kura semina kwa masheha na wajumbe wa masheha zimefanyika ambazo zinaendeshwa kila siku ya Jumanne ya kila wiki. Hadi sasa jumla ya shehia 132 za Unguja na Pemba zimeshapatiwa semina hizo. Tume itaendelea kuchukua juhudi zaidi ili kutoa elimu kwa umma.

Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar

Agizo Nam.1. Kamati imetaka Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar kuchukua wataalamu kwenye makampuni mengine ndani na nje ya Zanzibar ili kufidia pengo la ukosefu wa utaalamu wanaohitajika kiwandani hapo. Kwa kutengeneza mazingira mazuri katika maslahi watakayoyapata na kuwapatia motisha nyengine za kiutendaji kama mikataba ya kudumu na bonus ili kuendelea kuwabakisha kiwandani hapo kwa muda mrefu zaidi.

Utekelezaji

Wakala wa Uchapaji wa Serikali katika mwaka wa fedha 2016/2017 umeajiri wafanyakazi saba ambao ni wataalamu wa fani mbali mbali kwa mkataba wa miaka minne kwa vipindi vya miaka miwili miwili. Miongoni mwa wafanyakazi hao ni msimamizi na mshauri wa uendeshaji wa kiwanda mmoja, waendeshaji wa mitambo ya uchapishaji ya kisasa watano, na msarifu wa machapisho mmoja. Aidha, serikali imeajiri wafanyakazi wapya 18 wa fani mbali mbali ikiwemo uendeshaji wa mitambo, masuala ya mazingira, uhandisi na biashara ili kuongeza kasi na ufanisi katika shughuli za kiutawala na kiufundi kwa wakala.

Mhe. Mwenyekiti, wakala pia unatarajia kuongeza wataalamu wengine katika fani za uendeshaji mitambo na uchapaji na fani ya usarifu wa machapisho ili kuongeza uwezo wa uchapaji katika kukabiliana na kazi nyingi zinazotarajiwa kupatikana kutokana na mikakati ya wakala wa kutanua masoko ya shughuli za uchapaji.

Mhe. Mwenyekiti, ieleweke kwamba serikali ina dhamira kubwa ya kuendeleza Kiwanda cha Wakala wa Serikali wa Uchapaji ili kukidhi mahitaji yake ikiwemo wataalamu na kwa mwaka

huu fedha 2017/2018 serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni moja na nusu kuwa ni mtaji wa kiwanda hicho. Hata hivyo, Mhe. Mwenyekiti tayari Wizara ya Fedha na Mipango imetupatia bilioni 1 kwa ajili ya shughuli hizo.

Agizo Nam.2. Kamati imeshauri kujengwa kwa ghala jipya la Kiwanda cha Upigaji Chapa ambalo litakuwa na nafasi ya kutosha inayoendana na ukubwa wa kiwanda hicho kwa sasa. Kamati imesisitiza pia katika mchakato wa bajeti ijayo ujenzi wa ghala hilo upewe kipaumbele kwani kiwanda kimeshaanza kufanya kazi. Hivyo suala la kuwa na ghala lenye nafasi ya kutosha ni suala lisiloepukika ni jambo linalohitaji uendelezaji wa haraka.

Utekelezaji

Wakala wa Serikali wa Uchapaji katika mwaka huu wa fedha wa 2017/2018 umepanga kuanza hatua za mwanzo za kuandaa michoro ya ramani ya ghala kuu na makadirio ya gharama za ujenzi wa ghala hilo la kuhifadhia malighafi na vifaa vya uchapishaji kwa ajili ya kiwanda.

Agizo Nam.3. Kamati imeshauri kufanyika kwa zoezi maalum lna kukitangaza kiwanda hicho kwa umma kwa ajili ya kuongeza wateja na uelewa juu ya ubora wa huduma za uchapaji wa matoleo mbali mbali zinazopatikana kwa sasa.

Utekelezaji

Mhe. Mwenyekiti, wakala tayari unatekeleza mpango wa kujitangaza kwa shughuli za uchapaji ndani ya Zanzibar na Tanzania Bara kupitia vyombo vya habari vya redio na televisheni, maigizo na kushirikiana katika maoneshe mbali mbali ya ndani na nje ya nchi.

Agizo Nam.4. Kamati imeagiza Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kutoa toleo maalum kwa wizara, idara na taasisi zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar linalotaka na kuwahimiza kupeleka kazi zao zote za uchapaji katika Kiwanda cha Uchapaji cha Serikali zikiambatana na malipo halisi ya kazi hizo ili kuongeza utendaji kazi na uzalishaji kiwandani hapo na yeyote atakayekaidi agizo hilo hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi yake. Sambamba na taasisi zenye madeni kufanya utaratibu wa haraka kulipa madeni yao ili kiwanda kiweze kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi.

Utekelezaji

Mhe. Mwenyekiti, serikali imeshatoa maelekezo kwa wizara na taasisi zote za serikali ya kuzingatia kupeleka kazi zote cha uchapaji kwa wakala wa serikali wa uchapaji. Kwa kiasi kikubwa agizo hili la serikali hivi sasa linatekelezwa na wizara na taasisi za serikali. Aidha, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imewasilisha serikalini taarifa zote zinazohusu madeni ya wakala wa serikali wa uchapaji ili kuwepo kwa msukumo na utaratibu wa kulipwa deni hilo. Tayari serikali imetoa maelekezo kwa wizara na taasisi kulipa madeni hayo kupitia bajeti zao na baadhi ya wizara na taasisi zimeshaanza kulipa madeni hayo.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuweza kuendelea na jukumu lake la kuchapisha na kutoa huduma kwa muda wote, serikali imeitaka Wakala wa Serikali wa Uchapaji kutoa machapisho yake kwa ubora na kwa wakati ili kukidhi mahitaji ya wateja wao.

Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa

Agizo Nam.1. Kamati imeitaka wizara kuiongezea idara bajeti ya kutosha katika bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018 ili waweze kumalizia ujenzi unaoendelea wa ghala la maafa liliopo Unguja na kuanza kwa ujenzi wa ghala jipya kwa upande wa Pemba.

Utekelezaji

Mhe. Mwenyekiti, serikali imeongeza bajeti ya kamisheni ya kukabiliana na maafa kutoka shilingi milioni 850,867,000 kwa mwaka wa fedha 2016/2017 hadi shilingi bilioni 1,506,233,000 kwa mwaka fedha wa 2017/2018. Hili ni ongezeko la shilingi milioni 655,366,000 ambayo ni sawa na asilimia 77 ya bajeti ya 2016/2017. Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ilitekeleza mradi wa ujenzi wa kituo cha operesheni ya dharura kilichopo Maruhubi Unguja, ambacho pia kina sehemu ya ghala la kuhifadhia vifaa vya kukabiliana na maafa.

Kwa upande wa Pemba ofisi inaendelea kulitumia eneo katika jengo la uwanja wa Gombani kwa kuhifadhia vifaa vya kimaafa baada ya kulifanyia matengenezo makubwa ili liweze kukidhi haja hiyo. Hata hivyo, ofisi pia inaendelea na utaratibu wa kupata eneo maalum la kujenga ghala lake kwa matumizi hayo.

Agizo Nam.2. Kamati imeshauri kuwepo kwa zoezi endelevu la kupokea michango ya kifedha, vifaa kutoka kwa watu na wahisani mbali mbali ili kuweza kukabiliana na maafa kwa ufanisi zaidi badala ya kuanza kutafuta misaada hiyo wakati wa maafa yakishatokea. Na ni vyema kukawepo na *account* maalum ya michango ya maafa itakayotumika mara kwa mara kabla ya kupata misaada kutoka kwa wahisani wengine.

Utekelezaji

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais umefungua account maalum katika Benki ya Watu wa Zanzibar inayojuulikana kwa jina la *Zanzibar Disaster Fund* yenye Nam.051103000013 ambayo hupata michango kutoka kwa jumuiya, taasisi binafsi na watu mbali mbali kwa ajili ya kusaidia huduma mbali mbali wakati wa operesheni za maafa. Hata hivyo, licha ya kuwepo kwa account hiyo bado serikali itaendelea na utaratibu wake wa kutoa huduma na kuratibu operesheni za maafa wakati yanapotokezea.

Agizo Nam.3. Kamati imeshauri kutafutwa kwa eneo maalum ambalo litatumika kuhifadhia wahanga wa maafa makubwa yoyote yatakayotokea badala ya kutumia madarasa ya skuli na kuwakosesha wanafunzi masomo kwa kipindi husika.

Utekelezaji

Mhe. Mwenyekiti, Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa inaendelea kufanya mazungumzo na kamati za kukabiliana na maafa za Wilaya juu ya kutenga maeneo salama ya kuwahifadhia wahanga wa maafa katika maeneo yao. Hata hivyo, kama zilivyo taratibu za kusimamia masuala ya maafa ulimwenguni, suala la matumizi ya majengo ya umma mfano skuli, misikiti, makanisa na maeneo mengine ya umma wakati wa hali ya dharura kwa ajili ya kuhami maisha ya watu watakaoathirika kuwa haliepukiki wakati wa mamlaka zinazosimamia masuala ya maafa zikiwa zinaratibu namna ya kuwaweka watu hao katika maeneo yaliyotengwa.

Tume ya UKIMWI Zanzibar

Agizo Nam.1. Kamati imeshauri kuwa wizara na serikali kwa ujumla kuharakisha upatikanaji wa huduma ya bima ya afya kwa watumishi wake, kwani suala la bima ya afya haliwasaidia waathirika peke yake isipokuwa watumishi wote wa umma.

Utekelezaji

Mhe. Mwenyekiti, suala la kuanzishwa kwa bima ya afya hapa Zanzibar linafanyiwa kazi na wizara inayohusika na tayari imeshaandaa taratibu mbali mbali ili kuweza kuwasilisha hatua mbali mbali za kiserikali. Zipo taratibu nyengine za kiserikali zitafikiwa kabla ya kufikishwa kwenye Baraza la Wawakilishi ili suala hilo la bima ya afya liweze kukubalika. Kuna taratibu ambazo zitatakiwa zifatwe kabla ya kufikia uamuzi huo.

Agizo Nam.2. Kamati imeshauri Tume ya UKIMWI Zanzibar kulipa kipaumbele suala la utoaji elimu na kuendelea na utoaji wa elimu na kuhamasisha umma juu ya athari za virusi vya UKIMWI na wasibweteke kutokana na takwimu kuonesha kupungua kwa maambukizi ya UKIMWI Zanzibar.

Utekelezaji
Tume ya UKIMWI inaendelea kuelimisha jamii juu ya VVU na UKIMWI na athari zake kwa kutumia njia tofauti kama ifuatavyo.

a) Tume imekuwa ikitoa elimu kwa wafanyakazi kutoka sekta binafsi, wizara na taasisi za serikali juu ya VVU na UKIMWI na kuhamasisha kuanzisha programu za elimu ya VVU katika sehemu za kazi zinalenga wafanyakazi, familia zao na makundi ya watu wanaopokea huduma kutoka kwao.

b) Tume inaendelea kuwajengea uwezo vijana kitaaluma juu ya masuala ya UKIMWI na kuwawezesha kuwafikia vijana wenzao kwa ajili ya kuwapatia elimu juu ya VVU na UKIMWI pamoja na afya ya uzazi. Kwa kipindi cha mwaka 2016/2017 zaidi ya vijana 2000 wa Wilaya ya Kaskazini “A” Unguja na Micheweni Pemba walifikiwa. Wilaya hizi zilichaguliwa kutokana na tathmini iliyofanywa kuonesha kuwa katika Wilaya hizi kuna kiwango kidogo cha uelewa wa masuala ya VVU na UKIMWI na afya ya uzazi kwa vijana wa Wilaya hizo.

c) Viongozi wa dini ya Kiislamu na Kikiristo wamekuwa wakipatiwa elimu ya VVU na UKIMWI na udhalilishaji wa jinsia ili na wao wawaelimisha waumini wao kupitia taasisi za kidini katika Misikiti, Makanisa, madarasa na mihadhara.

d) Tume imekuwa ikitoa elimu juu ya VVU, UKIMWI, udhalilishaji wa kijinsia, afya ya uzazi, sheria ya UKIMWI kupitia njia a redio na televisheni zikiwemo redio jamii. Vile vile tume inaandaa vipeperushi vya aina mbali mbali vyenye ujumbe wa kuelimisha na kutanabahisha jamii juu ya huduma zinazopatikana nchini zinazohusiana na maradhi ya UKIMWI.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala hili Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein ameshatoa maelekezo ya kina ambapo amesisitiza suala la kutolewa elimu kwa umma ili kuongeza mwamko wao juu ya maradhi ya UKIMWI kama ilivyokuwa katika miaka ya mwanzoni wakati wa maradhi haya yanaingia hapa nchini. Hii ni kwa sababu jamii yetu imekuwa kama imesahau juu ya UKIMWI kwa kuwa uhamasishaji umekuwa mdogo, hatua zitachukuliwa ili uhamasishaji uwe mkubwa kuhakikisha tunapambana na maradhi haya thakili.

Agizo Nam.3. Kamati imeshauri Tume ya UKIMWI Zanzibar na serikali kwa ujumla kutafuta namna ya kuzipa ruzuku taasisi kama *ZIFA+* ambazo zinajihusisha na kuwasaidia waathirika wengi wa UKIMWI kama inavyopatiwa ruzuku kwa nyumba za kurekebisha tabia Sobha House.

Utekelezaji

Mhe. Mwenyekiti, moja kati ya majukumu ya Tume ya UKIMWI ni kutafuta rasilimali kwa ajili ya utekelezaji wa muitikio wa VVU na UKIMWI nchini ikiwemo kuwapatia fedha wahusika muhimu katika harakati za mapambano dhidi ya UKIMWI. Jumuiya ya watu wanaoishi na VVU *ZIFA+* ni miongoni mwa wahusika wakubwa wa mapambano dhidi ya UKIMWI ambayo tume inafanya kazi nao kwa karibu sana. Tume imeipatia fedha *ZIFA+* kwa ajili ya utekelezaji wa baadhi ya kazi zake kwa mwaka wa fedha 2016/2017, *ZIFA+* walipatiwa shilingi milioni 3,000,000 kwa ajili ya kazi za uratibu wa shughuli zao. Aidha, tume imekuwa na utaratibu wa kuweka fedha na kuwapatia katika bajeti ya kila mwaka kadiri ya hali inavyoruhusu.

Mhe. Mwenyekiti, tume pia kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo imekuwa ikitoa aina nyengine za misaada kwa jumuiya hizi ili kuweza kutekeleza majukumu yao na kutoa huduma bora kwa walengwa.

Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ, SMT na Masuala ya Muungano pamoja na Programu ya *TASAF III*

Agizo Nam.1. Kamati imeshauri kutolewa kwa elimu ya kutosha kwa walengwa wa miradi ya *TASAF* kabla ya zoezi lolote la mradi husika kuanza, ili walengwa hao wapate uelewa wa kutosha wa miradi husika.

Utekelezaji

Mhe. Mwenyekiti, *TASAF* Zanzibar kupitia Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali ina utaratibu wa kutoa elimu ya kutosha kwa walengwa wa programu hiyo wa kaya masikini kabla ya zoezi lote la kazi za miradi kuanza, ikiwemo kazi za kutoa ajira za muda. Malipo ya kaya masikini pamoja na vikundi vya kuweka na kuwekeza kwa Unguja na Pemba. Shughuli hii

hufanywa na wasimamizi wa mradi ambao ni watendaji wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, watendaji wa Wilaya pamoja na wataalamu wa *TASAF* kutoka Makao Makuu ili kujenga uelewa kwa wananchi kwa kiasi kikubwa lengo hili limefanikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, zoezi la kutoa elimu endelevu na serikali itaendelea kuwasaidia wahusika kuelewa adhma ya serikali kufikisha huduma ya mfuko huu kwa wawili wao wajitahidi kusaidia lengo hilo kufikiwa.

Agizo Nam.2. Kamati imeagiza kufanyika upya kwa uhakiki yakinifu wa *TASAF III* ili kuwabaini watu wasio na sifa walioingizwa na kunufaika na mradi huo na kuwaacha wale wenye sifa na baada ya kuhakiki, uhakiki huo waingizwe ili wao waweze kunufaika kwani kamati ina amini bado wapo watu wanaonufaika na mradi wa kunusuru kaya masikini bila ya kuwa na sifa stahiki na kuwakosesha kupata haki wale ambao wamekusudiwa.

Utekelezaji

Mhe. Mwenyekiti, ofisi imeshafanya uhakiki yakinifu kwa lengo la kubaini uwepo wa watu ambao wana sifa na wasiokuwa na sifa yakuwepo kwenye mpango wa kunusuru kaya masikini. Pia inaendelea kuwaorodhesha wale ambao wana sifa ya kuingizwa kwenye mpango wa kaya masikini hususan watoto wanaotimiza masharti ya afya na elimu. Vile vile *TASAF* huwaondoa katika mpango walengwa waliofariki na kuingizwa walengwa wapya ambao wanastahiki kuwepo katika mpango huo. Zoezi hilo ni endelevu.

Agizo Nam.3. Kamati imeshauri kuwepo na utaratibu wa mpango maalum wa kufanya ukaguzi wa miradi ya *TASAF I* na *TASAF II* iliyokamilika na kukabidhiwa kwa sekta husika ili miradi hiyo isiwe imetelekezwa na kukosa kufanyiwa hata matengenezo madogo pale inapotokea kuwa na hitilafu. Aidha, kamati inazitaka wizara husika zinapokabidhiwa miradi ya *TASAF* waitunze miradi hiyo na waendeleze miradi hiyo kwa faida ya wananchi wetu.

Utekelezaji

Mhe. Mwenyekiti, utaratibu uliokuwepo katika utekelezaji wa programu ya *TASAF I* na *TASAF II* kwa Tanzania nzima ni kuwa na miradi yote iliyotekelezwa ikabidhiwe kwa wizara husika na sekta ya mradi huo kwa ajili ya kusimamia na kuendeleza kwa mujibu wa mazingira ya mradi. Hivyo, miradi yote iliyobuniwa na kutekelezwa katika programu ya *TASAF I* na *TASAF II* yote imekabidhishwa kwa wizara zinazohusika na sekta zenye miradi. Ni jukumu la wizara hizo kusimamia na kufuatilia miradi hiyo ili kuhakikisha kuwa inaendelea kutoa tija kwa wananchi kama ilivyokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, hata hivyo, ili kuhakikisha kuwa miradi hiyo inakuwa endelevu na kuendelea kuleta tija, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kushirikiana na uongozi wa *TASAF* inaendelea kuzikumbusha wizara juu ya haja ya kuendeleza miradi hiyo, kwa kuzishauri njia bora za kusimamia shughuli za miradi hiyo husika.

Ofisi ya Uratibu wa Shughuli za SMZ Dar es Salaam

Agizo Nam. 1: Kamati imeagiza kufanywa kwa matengenezo makubwa na haraka ya ukarabati mkubwa wa jengo la uratibu wa shughuli za SMZ Dar es Salaam, pamoja na mazingira yanayozunguka jengo kutokana na kuhofia kuhamishwa ndani ya maeneo hayo muhimu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ukizingatia kwamba ofisi hii ndio ofisi pekee ya SMZ kwa upande wa Tanzania Bara.

Utekelezaji

Mhe. Mwenyekiti, serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais tayari ina mpango wa muda mrefu wa kulijenga jengo la Ofisi ya Uratibu wa SMZ liliopo Dar es Salaam. Serikali tayari imeanza maandalizi ya mpango huo ambapo tayari imewasiliana na taasisi zake za kifedha ili kusaidia utekelezaji wa mpango huo wa serikali. Makusudio ya ujenzi huo ni kujenga jengo ambalo litajumuisha uwepo wa ofisi nyengine za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Vile vile Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais katika mpango wake wa muda mfupi imepanga kufanya matengenezo madogo madogo ikiwemo kupaka rangi, uezekaji wa paa kupitia bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018 kwa kutenga jumla ya shilingi 24 milioni.

Aidha, ofisi katika mwaka wa fedha 2016/2017 imelifanyia matengenezo jengo hilo katika mazingira yake ya nje ikiwemo utengenezaji wa bustani, sehemu ya kuweka gari na sehemu ya kuchomea taka.

Agizo Nam. 2: Kamati imeagiza kuwepo kwa sera maalum ikiwemo mikakati ya lazima itakayowafanya viongozi wa wizara na taasisi za Zanzibar kuitumia vizuri kikazi Ofisi ya Uratibu wa Shughuli za SMZ iliopo Dar es Salaam, ili kuwepo na ufuatilaji na upatikanaji wa taarifa zinazokuja kuwasilishwa katika vikao mbali mbali.

Utekelezaji

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Uratibu wa Shughuli za SMZ Dar es Salaam imekuwa ikitumiwa na viongozi mbali mbali wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ajili ya utekelezaji majukumu yao wanapokuwa Dar es Salaam, ikiwemo shughuli za ufuatiliaji, upatikanaji wa taarifa zinazokuja kuwasilishwa katika vikao vya serikali. Aidha, ofisi hivi sasa imekuwa ni muhimu kwa wizara zinazohitaji kukutana na wizara wenza za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vile vile karibu kamati zote za Baraza la Wawakilishi Zanzibar zinatumia ofisi hii kuwaunganisha na ofisi zote wanazohitaji kukutana nazo kulingana na ziara na malengo ya kamati husika.

Ofisi pia hutumika kama kiunganishi kwa viongozi wanaposafiri kuelekea mikoa mengine ya Tanzania Bara hata nje ya nchi. Kuongezeka kwa watumiaji wa matumizi ya ofisi hii kunatokana na maelekezo na azma ya serikali ya kuongeza wigo kwa huduma zinazotolewa pamoja na shughuli zinazofanywa na ofisi hii kuwa na tija sambamba na kurahisisha utekelezaji wa shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar huko Tanzania Bara. Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa ili kuipa nguvu zaidi kiutendaji ofisi hii ni kuipa hadhi zaidi kwa kuifanya kuwa ofisi ya uratibu kutoka ngazi ya idara pamoja na kuongezea bajeti yake.

Agizo Nam. 3: Kamati imetaka Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kuipatia ofisi hii fedha za kutosha kwa ajili ya matumizi ya kawaida (*OC*) na kwa wakati muwafaka na kuingizwa moja

kwa moja kwenye *account* yao kinyume na inavyofanyika kwa sasa. Aidha, ofisi ipatiwe vitendea kazi vya kutosha na vya kisasa ili wafanyakazi waweze kutekeleza kazi zao kwa ufanisi mkubwa.

Utekelezaji

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Uratibu wa Shughuli za SMZ Dar es Salaam kwa mwaka huu wa fedha 2017/2018 imeidhinishiwa jumla shilingi 542,930,000 ikiwa na ongezeko la shilingi 95,413,000 kwa bajeti ya mwaka 2016/2017 ambayo ilikuwa shilingi 447,517,000.

Aidha, kama ilivyo kwa idara nyengine za serikali kwa mwaka huu wa fedha Ofisi ya Uratibu Shughuli za SMZ Dar es Salaam imepatiwa asilimia mia moja ya fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida (*OC*) kwa kila mwezi, kama ilivyoidhinishwa katika *cash flow* yao. Hivyo, Ofisi ya Uratibu wa Shughuli za SMZ Dar es Salaam imepata asilimia 100 ya fedha kwa matumizi ya kawaida kwa mwezi wa Julai na Ogosti katika fedha zilizoombwa. Kwa upande wa upatikanaji wa vitendea kazi katika mwaka wa fedha 2017/2018, ofisi imetenga jumla ya shilingi 10,653,000 kwa ajili ya ununuzi wa kompyuta, *scanner, projector* na *television* ambazo nazo zinapatikana kama ilivyopangwa katika *cash flow*.

Agizo Nam. 4: Kupatiwa mafunzo nayaoendana na majukumu ya hadhi ya ofisi ukizingatia matumizi ya ofrisi hii kwa viongozi mbali mbali ikiwa pamoja na mabalozi na viongozi wakuu wa nchi za nje.

Utekelezaji

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Uratibu wa Shughuli za SMZ dar es Salaam katika mwaka wa fedha 2017/2018 imetenga jumla ya shilingi 13,240,000 kwa ajili ya mafunzo ya muda mfupi kwa maofisa wanne wakiwemo maafisa uratibu na wafanyakazi wa kada nyengine ili kuongeza ufanisi wa majukumu yao ya kazi. Maofisa hawa watahudhuria mafunzo kwa zamu kwa kila robo mwaka na mafunzo hayo kwa maofisa waratibu yamejikita katika nyanja za kidiplomasia na uhusiano wa kimataifa.

Idara ya Watu wenye Ulemavu

Agizo Nam. 1: Kamati imeishauri wizara kuipatia Idara ya Watu wenye Ulemavu bajeti itakayokidhi mahitaji ya utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi, ukizingatia idara hii ni muhimu katika kufuatilia shughuli mbali mbali zilizofanywa na watu wenye ulemavu wa aina mbali mbali.

Utekelezaji

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza agizo hili serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018, imeongezea bajeti Idara ya Watu wenye Ulemavu kufikia shilingi 498,832,000 kutoka shilingi 462,121,300 za mwaka wa fedha 2016/2017, ili kurahisisha ufuatiliaji wa shughuli za idara katika maeneo mbali mbali.

Agizo Nam. 2: Kamati imeagiza Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kutafuta namna ya kuwapatia usafiri japo wa gari nyengine moja kwa ajili ya kazi za ufuatiliaji wa kazi za kila siku sambamba na kuwapatia vitendea kazi ili wafanye kazi zao kwa ufanisi mkubwa.

Utekelezaji

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imetekeleza agizo hili kwa kuipatia gari moja Idara ya Watu wenye Ulemavu kwa ajili ya ufuatiliaji wa shughuli zao za kila siku. Aidha, kwa huu wa fedha Idara ya Watu wenye Ulemavu imetenga jumla ya shilingi 10,000,000 kwa ajili ya unuuzi wa vifaa vya kufanyia kazi ikiwemo kompyuta na vifaa vyake. Kutokana na utaratibu kwa kila idara kupatiwa fedha kwa mujibu wa mahitaji yake, hadi mwishoni mwa mwezi wa agosti 2017 idara tayari imenunua kompyuta mbili na imeshaanza kuzitumia.

Agizo Na. 3: Kamati imeshauri kuwepo na uhusiano wa karibu baina ya Idara ya Watu wenye Ulemavu na Idara ya Uwezeshaji Kiuchumi kwa kuwapa kipaumbele watu wenye ulemavu kwenye masuala ya uwezeshaji ili kuwainua kiuchumi kupitia vikundi vyao vya ushirika.

Utekelezaji

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imekuwa ikishirikiana na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana na Wanawake na Watoto katika kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanapewa kipaumbele maalum katika huduma zinazotolewa na wizara hiyo. Miongoni mwa huduma zinazotolewa kwa watu wenye ulemavu ni kuwapatia mafunzo ya ujasiriamali kwa lengo la kuwajengea uwezo ili kuweza kufanya shughuli zao za kibiashara kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, ofisi pia imekuwa ikishauriana na wizara hiyo juu ya kuwaunganisha moja kwa moja na watu wenye ulemavu kwa kupitia vikundi vyao ili kuweza kupata mikopo ya kuendeleza shughuli zao. Katika kurahisisha utekelezaji wa shauri hilo, wizara inayohusika na masuala ya uwezeshaji imeteuwa mjumbe kutoka Idara ya Watu wenye Ulemavu kuwa miongoni mwa wajumbe wa bodi ya mikopo ya uwezeshaji. *(Makofi)*

Agizo Nam. 4: Kamati imeshauri Idara ya Watu wenye Ulemavu na serikali kwa ujumla kulitilia mkazo suala la kuweka miundombinu rafiki itakayokidhi mahitaji ya watu wenye ulemavu katika majengo ya zamani na mapya yanayoendelea kujengwa na serikali.

Utekelezaji

Idara ya Watu wenye Ulemavu imeshaandaa dodoso pamoja na ratiba ya ukaguzi wa majengo yote ya serikali katika Mkoa wa Mjini Magharibi ili kugundua majengo yasiyofikika, shughuli hii ilianza tarehe 3 Septemba, 2017 ambapo taarifa zinazopatikana zitakuwa ni chanzo cha kuendeleza ukubwa wa tatizo hili hivi sasa na kupendekeza njia sahihi za kushughulikia suala hili. Aidha, idara kwa kushirikiana na Jumuiya za *ZACEDID* imeandaa muongozo wa ujenzi utakaozingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu. Muongozo huo tayari umewasilishwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa ajili ya hatua zinazofuata.

Mhe. Mwenyekiti, suala la kuwepo kwa miundombinu itakayokidhi mahitaji ya watu wenye ulemavu imekuwa ni moja kati ya masuala muhimu ambayo serikali imeyapa kipaumbele na limo katika mipango yake. Serikali itaendelea kulisimamia ili watu wenye ulemavu waweze kutumia miundombinu hiyo bila ya vikwazo.

Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa

Agizo: Kamati imeagiza kutafuta namna ya kupata fedha kwa ajili ya kununua vifaa vipya vya kisasa ambavyo vitatumika katika shughuli za sherehe mbali mbali za kitaifa, lakini pia vitatumika kufanyia biashara ya kuwakodisha watu binafsi kwa ajili ya kuongiza mapato serikalini.

Utekelezaji

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018 serikali imeongeza bajeti ya Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa kutoka shilngi 920,000,000 za mwaka 2016/2017 hadi kufikia shilingi 950,000,000. Lengo la ongezeko hilo la bajeti ni kuiwezesha idara kutekeleza majukumu yake ya msingi, kuratibu sherehe za maadhimisho ya kitaifa kwa ufanisi mkubwa ikiwa ni pamoja na kununua vifaa mbali mbali vitakavyotumika katika sherehe za kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kupitia Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pia inatumia baadhi ya vifaa hivyo kuwakodisha watu na taasisi mbali mbali za serikali, za binafsi na hivyo huchangia katika kukusanya mapato ambayo ofisi imepangiwa. Kwa mwaka huu wa fedha Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kupitia Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa imepangiwa kukusanya shilingi 32,521,000.

Hitimisho:

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais itaendelea kupokea ushauri na maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa na kuyafanyia kazi ipasavyo. Kwani ushauri na miongozo hiyo inatusaidia sana kuongeza kasi na umakini katika utekelezaji wa majukumu yetu na serikali kwa jumla.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumalizia naomba tena nirudie kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu kwa kunisikiliza kwa makini na naamini wataipokea ripoti yetu kwa nia ya kuendelea kujenga ushirikiano na umoja katika chombo hiki ili kuleta manufaa zaidi kwa wananchi wetu.

Baada ya maelezo hayo kwa heshima kubwa naomba kutoa hoja Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Omar Seif Abeid (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kutoa maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusiana na utekelezaji wa maagizo ya kamati ya mwaka 2016/2017 kwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kupeleka shukurani zangu za dhati kwa mwingi wa rehema, mwenye utukufu, kwa kutujaalia pumzi na afya njema na kuweza kutukutanisha tena katika Baraza hili tukufu, kwa lengo la kuendelea kuwatumikia wananchi wetu wa Zanzibar. Aidha, natumia fursa hii kukushukuru na kukupongeza wewe kwa namna unavyoliongoza Baraza hili kwa uweledi mkubwa uliojaa busara na hekima wakati unapoliongoza Baraza lako, ni imani yangu kwamba, utaendelea kuliongoza Baraza hili kwa uadilifu wa hali ya juu wewe na wasaidizi wako kwa lengo la kuimarisha demokrasia katika chombo hiki.

Mhe. Mwenyekiti, pia nachukua fursa hii kumshukuru kwa dhati ya moyo wangu Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohammed Shein, kwa kuiongoza nchi yetu kwa hekima, busara na uadilifu mkubwa kwa kipindi chake chote tokea kushika nafasi ya uraisi kwa kipindi chote cha utumishi wake wa urais. Hekima na Busara zake anazozitumia katika kuongoza nchi yetu, ndizo ambazo zimetufanya hadi leo kuweza kuishi kwa amani, umoja na utulivu wa hali ya juu. Tunakuomba Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema umzidishie busara zaidi ili azidi kutuongoza kwa umakini na kufikia malengo tulilolikusudia.

Pia sina budi pia kumshukuru na kumpongeza sana Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, kwa umahiri wake mkubwa wa kuyasimamia vyema majukumu ya wizara zote za serikali na kumsaidia kwa umakini mkubwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, hivyo kuweza kufikia malengo tuliyoyakusudia ya kuwatumikia wananchi wetu utumishi ulio bora na wenye imani na ni imani yangu kwamba wananchi wetu wa Zanzibar kwa ujumla wao wanafurahia kazi kubwa zinazofanywa na serikali yetu ambayo inasimamia sera za Chama cha Mapinduzi.

Vile vile nachukua fursa hii kumshukuru sana Waziri wa Nchi, Ofisi Makamu wa Pili wa Rais, Mhe.Mohammed Aboud Mohammed pamoja na watendaji wake wote, wakiongozwa na Katibu Mkuu wa wizara hiyo, kwa mashirikiano waliyotupatia wakati wa kuzipitia taarifa za utekelezaji wa wizara hii. Mashirikiano wanayotupatia ndio moja kati ya sababu kubwa kwamba kamati yetu kuweza kukamilisha kazi iliyojipangia bila ya kikwazo.

Mhe. Mwenyekiti, sina budi kutumia fursa hii kumpongeza kwa dhati Dkt. Idrisa Muslim Hija kwa kuteuliwa kwake kuwa Katibu Mkuu katika wizara hii. Namtakia kila la kheri na mafanikio katika kutekeleza majukumu yake mapya aliyokabidhiwa ya kila siku. Ni imani yangu kwamba kamati yetu kwa umahiri wake mkubwa ataweza kupokea kijiti alichokabidhiwa na mtangulizi wake na ataweza kuitumikia wizara hii na kuifikishia malengo yaliyokusudiwa ya kuwatumikia wananchi wetu wa Zanzibar, ukitilia maanani kwamba wizara aliyokabidhiwa ndio mama wa wizara nyengine za serikali yetu.

Pia kwa namna ya pekee, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa kazi zao nzuri wanazozifanya wakati wote wa kazi za kamati, jambo ambalo imekuwa ni wepesi kwangu kuweza kuiongoza kamati hii. Wajumbe wameonesha umahiri mkubwa na umakini wa hali ya juu na wameweza kuijadili ipasavyo taarifa hii ya utekelezaji na kuhoji mambo mengi ya msingi, kwa lengo la kuhakikisha kwamba fedha zinazoidhinishwa katika Baraza hili zinatumika vizuri na kwa maslahi mapana kwa ajili ya wananchi wetu wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii pia, kuwapongeza na kuwashukuru Wawakilishi wote waliomo katika Baraza lako tukufu kwa kuendelea kuwawakilisha na kuwatumikia wananchi waliowachagua. Ni wazi kwamba wananchi wamejenga imani kubwa kwetu, nasi hatuna budi kurejesha imani hiyo kwao, kwa kuwatumikia kwa moyo wetu wote kwa dhamira ile ile ya kuleta maendeleo ya nchi yetu kwa ajili ya maslahi ya wananchi wetu wote tunaowawakilisha katika Baraza hili tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuendelea na hotuba hii, kwa ruhusa yako na kwa heshima ya kipekee naomba niwatambua Wajumbe wa Kamati yangu ya Kusismamaia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Omar Seif Abeid	Mwenyekiti
2.	Mhe. Panya Ali Abdallah	M/Mwenyekiti
3.	Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Mjumbe
4.	Mhe. Ame Haji Ali	Mjumbe
5.	Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Mjumbe
6.	Mhe. Mussa Ali Mussa	Mjumbe

Aidha Kamati hii inafanyakazi na makatibu wawili ambao wamekuwa wakitusaidia na kutushauri kwa karibu sana na kwa kiasi kikubwa na kwa uweledi wa hali ya juu katika kutekeleza majukumu yetu ambayo yametupatia Kamati hii heshima na mafanikio makubwa ya namna ya kipekee. Makatibu hao ni:-

1.	Ndg. Karima Abdul-Wahab	Katibu
2.	Ndg. Enzi Talib Enzi	Katibu

Mhe. Mwenyekiti, Ni jambo la lazima kwa kila wizara kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati katika Mkutano wa Baraza wa mwezi wa Oktoba kwa kila mwaka. Kwa mujibu wa Kanuni ya 108(15) Taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ni lazima kwanza iwasilishwe katika Kamati za Kudumu za Baraza zinayosimamia Wizara hizo kabla ya kuwasilishwa kwenye Baraza zima. Kwa hivyo, Kamati ya Kusimamia Viongozi wakuu wa Kitaifa inawasilisha leo mbele yako Baraza lako tukufu taarifa hiyo ikiwa ni utekelezaji wa wajibu wake kwa mujibu wa Kanuni ya 108(14) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi**.**

Mhe. Mwenyekiti, Taarifa hii ya utekelezaji inatokana na Maagizo ya Kamati yaliyojitokeza baada Kamati kuwasilisha ripoti yake ya utekelezaji wa wizara na kujadiliwa na Baraza katika Mkutano wa Mwezi Febuari.

Katika Bajeti ya 2016/17 Kamati yangu ilitoa maagizo kadhaa kwa Taasisi inazozisimamia. Hivyo chini ya Wizara ya Afisi ya Makamu wa Pili. Taarifa hii inatoa hali halisi ya utekelezaji wa maagizo hayo, Kwa upande wa ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka wa fedha 2016/17 iliagizwa na Kamati kutekeleza maagizo Thelathini na tatu (33) ambayo yalielekezwa kuchukuliwa hatua kupitia idara tofauti, ambapo kwa mgawanyo wa Kiidara ni kama ifuatavyo:

i) Tume ya Kitaifa ya Uratibu wa Dawa za kulevya, Maagizo saba (7)
ii) Tume ya Uchaguzi, maagizo matano (5)
iii) Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar, Maagizo manne (4)
iv) Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa, maagizo matatu (3)

v) Tume ya UKIMWI, maagizo matatu (3),
vi) Idara ya Uratibu wa Masuala ya SMZ na SMT na masuala ya Muungano, maagizo matatu (3)
vii) Afisi ya Uratibu wa shughuli za SMZ -Dar es Salaam. Maagizo manne (4)
viii) Idara ya watu wenye ulemavu Maagizo manne (4)
ix) Idara ya sherehe na maadhimisho ya Kitaifa. Agizo moja (1)

Mhe. Mwenyekiti, Baada ya kupokea Taarifa ya Utekelezaji wa Wizara Kamati ilichambua hayo maagizo ili kuona kwamba ilikuwa na maoni yafuatayo:

Kamati yangu inaipongeza sana serikali kwa ujumla wake na hususan inaipongeza Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais ambayo ndiyo msimamizi mkuu wa shughuli za serikali kwa kuona umuhimu wa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati na kuweza kutekeleza maagizo mengi yaliyotolewa na kamati kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi katika wizara hiyo na kuweza kutimiza azma ya serikali ya kuwaletea wananchi wake maendeleo. Aidha Kamati yangu inaipongeza Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kutambua umuhimu na kuheshimu maagizo ya Kamati hivyo kupelekea kuyatekeleza kwa vitendo dhana ya *check and balance* na kuona namna muhimili mmoja unavyofanya kazi kwa mashirikiano na muhimili mwengine wa dola.

Mhe. Mwenyekiti, Moja kati ya Maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwa Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais ni Serikali kuongoza Bajeti kwa taasisi zilizochini ya wizara hiyo ili ziweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Kamati yangu inapongeza sana serikali kwa kuona umuhimu wa kukubali ushauri wa Kamati wa kutaka kuongeza bajeti ya taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Tunaweza kusema kwa karibu idara zote zimepata ongezeko la kibajeti katika mwaka fedha 2017/18 ikilinganishwa na ile ya 2016/17.

Kwa upande wa kamati yetu tunaipongeza sana Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kufuata ushauri tuliowapa wa kuongeza bajeti kwa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais ambapo ndio wizara mama kama tulivyotangulia kusema.

Mhe. Mwenyekiti, Tume ya Kitaifa ya Uratibu na Udhibiti wa Madawa ya Kulevya. Tume hii imepata ongozeko la aslimia 36 ya bajeti ya mwaka wa fedha 2017/18. Hii inaonesha jinsi gani Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais ilivyoweza kulipa umuhimu suala la kupambana na dawa za kulevya jambo ambalo ni janga kubwa kwa jamii na linaloathiri nguvu kazi ya Taifa.

Aidha, Kamati inaipongeza Tume ya Kitaifa ya kudhibiti za kulevya kwa kuweza kutekeelza agizo la kuongeza kutanua wigo kwa utoaji wa elimu katika jamii kuhusu athari za matumizi ya dawa ya kulevya ambapo Tume ya Uratibu wa Udhibiti wa Dawa za Kulevya imeweza kuyafikia makundi mbali mbali ya kijamii na kutoa elimu juu ya madhara ya utumiaji wa dawa na athari kwa jamii yetu. Kamati imelithibitisha hili kwa vitendo wakati ilipokuwa inafanya ziara mbali mbali kukutana na makundi hayo na kupata ithibati kwa wanamakundi hao kwamba wamekuwa karibu sana na taasisi hii. Jambo ambalo limeleta faraja kubwa kwa Kamati. Tunaiomba idara inayosimamia shughuli za madawa ya kulevya iendelee kuwa karibu sana na jamii hii ili iendelee kutoa elimu. Jambo ambalo limeleta faraja kubwa.

Pia Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kupitia Tume ya Kitaifa ya Uratibu na Udhibiti wa Dawa za kulevya imeweza kutekeleza ipasavyo agizo la Kamati la kuzidisha mashirikiano wadau wengine katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya zikiwemo, Mahkama, Polisi, Mkemia Mkuu, *DPP* na Taasisi ya kupambana na Rushwa kwa kuweza kufanya mikutano ya pamoja kwa lengo la kuimarisha mapambano dhidi ya janga hilo.

Hata hivyo bado kamati haijaridhishwa na suala zima la mwenendo wa Kesi zinazohusiana na dawa za kulevya kutokana na kuwa watu wengi wanakamatwa na dawa za kulevya lakini

kushindwa kupatikana na hatia mahakamani na kuifanya jamii kutokupata hofu kwa jamii na kuendelea kutenda kosa hili la usafirishaji na uingizaji na matumiaji wa dawa za kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inashauri kutoa elimu zaidi kwa wadau wote wanaohusika na uendeshaji na usimamizi wa kesi za dawa za kulevya hasa wapelelezi kwani wao ndio msingi wa kujenga kesi kabla kufika mahakamani. Pia suala zima la usimamizi madhubuti katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya wakati wa utunzaji wa vielelezo nguvu zaidi zinahitajika na uaminifu zaidi unahitajika wakati huu juu ya kuvitunza vielelezo kabla ya kuvipeleka Mahakamani ili wakati vinapopelekewa Mahakamani vielelezo hivyo viwe ni thabiti kama vile ambavyo vilivyotoka kwa Mkemia Mkuu. Kufanya hivyo, kutaisaidia jamii yetu iweze kuona kwa vitendo kwamba serikali inalichukulia mapambano dhidi ya dawa ya kulevya ni vita vya kitaifa na jamii yote inastahili kushiriki katika vita hivyo. Ili kuhakikisha kwamba nchi yetu imeshinda vita dhidi ya wahalifu hao.

Mbali na utekelezaji wa maagizo hayo bado Kamati yangu inasisitiza kuendelea kutekeleza maagizo yaliyobaki ambayo yalitolewa na Kamati kwa idara hiyo likiwemo lile la kuimarisha upekuzi wa wasafiri katika vituo vya kuingilia na kutoka nchini ambavyo ni viwanja vya ndege na bandari pamoja na lile la kuweka mabango ya tahadhari katika maeneo yenye mkusanyiko mkubwa wa watu, mabango hayo yanatakiwa kuonesha madhara ya dawa za kulevya na adhabu inayotolewa kwa mtu atakayepatikana na hatia. Na Kufanya hivyo kutasaidia kujenga ghofu katika jamii na kuona kwamba namna gani serikali yetu ilivyochukua hatua dhidi ya mtu yeyote atakaejihusisha na makosa hayo anavyoweza kuchukuliwa hatua za kisheria dhidi ya uingizaji na utumiaji wa dawa za kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, Tume ya Uchaguzi, katika Tume hii Kamati ilikuwa na maagizo matano (5). Kamati inaipongeza Afisi ya Makamu wa Pili kwa kuanza kutekeleza maagizo ya Tume ya Uchaguzi likiwemo lile la kupatiwa kiwanja kilichopo karibu na Afisi ya Tume ya Uchaguzi, pamoja na kupatiwa jengo linalomilikiwa na Shirika ambalo kwa sasa agizo hilo tayari limeshatekelezwa. Hizi ni hatua nzuri zilizoanza kwa utekelezaji wa maagizo hayo na ni vyema zikapewa uzito unaostahiki ili kukamilika kwa haraka. Aidha, Kamati imeridhika na maelezo ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa jitihada iliyochukuwa ya kuyafanyia matengenezo magari ya Afisi ya Tume ya Uchaguzi na kuona umuhimu wa kutenga kiasi cha fedha za kununulia gari mpya katika mwaka wa fedha wa 2017/18. Nachukuwa fursa hii kuipongeza sana wizara kwa kuliona hilo.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaipongeza sana Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kupitia Tume ya Uchaguzi, kwa kutekeleza agizo la Kamati la kuwataka kuandaa vipindi mbali mbali vinavyotoa elimu kwa umma kuhusu kazi na majukumu ya Tume hiyo ikiwa ni pamoja na kueleza historia ya chaguzi za Zanzibar na uwepo wa Daftari la kudumu la wapiga kura. Hata hivyo Kamati imesisitiza kuzingatia muda mzuri wa kurusha vipindi hivyo hewani muda ambao watu wengi wataweza kupata fursa ya kusikiliza vipindi hivyo. Pia watapata muda ya kuangalia na kusikiliza ili taaluma ifike kwa watu walio wengi.

Aidha, Kamati inaendelea kusisitiza suala la Tume ya Uchaguzi kuwa na Afisi zake katika kila Wilaya ili kuwaondolea usumbufu wananchi wanaohitaji huduma za Afisi hiyo. Kamati inaitaka Afisi ya Makamu wa Pili kulipa uzito unaostahiki. Pamoja na kuwa kamati yangu inafahamu kwamba jambo hilo limeanzwa kutekelezwa kwa kiasi kikubwa.

Mhe. Mwenyekiti, Wakala wa Uchapaji ni Taasisi nyingine iliyo chini ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais ambayo Kamati yangu ilitoa maagizo manne (4) kwa Taasisi hiyo**.**

Kamati inaipongeza Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kupitia Wakala wa Uchapaji kwa kutekeleza maagizo ya Kamati kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi katika Taasisi hiyo.

Miongoni mwa maagizo yaliyotekelezwa vizuri ni lile la kuajiri wataalam wa fani tofauti katika kutekeleza majukumu ya Taasisi hiyo na kuweza kukabiliana na ushindani wa kibiashara. Aidha kamati inaeleza kuridhishwa kwake kwa namna ya kuanza kutekelezwa agizo lake la kujengwa ghala la kuhifadhiwa vifaa vya wakala, ambalo kwa sasa tayari michoro ya ghala hiyo imeshapatikana. Pia Kamati inapongeza jitihada za Wakala kutangaza kazi zake nje na ndani ya Zanzibar ambapo kamati imeona jitihada hizo za wakala wa Uchapaji pale walipoonesha dhamira ya kushirikiana na wakala wa Shirika la Magazeti ya Serikali Tanzania Bara kwa lengo la kutafuta soko la nje.

Sambamba na hilo Kamati inapongeza Wakala kwa jitihada zake za kujitangaza kupitia vyombo mbali mbali vya habari ndani na nje ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati pia imeridhishwa sana na jitihada za wizara ya kuzitaka Taasisi zote za Serikali kuchapisha kazi zao katika Wakala mkuu wa uchapaji wa Serikali. Hata hivyo, Kamati inasisitiza kwamba kila Taasisi ya Serikali inayopeleka kazi zake kwa wakala kuweza kulipa fedha zake zinazostahiki kwa na wakati.

Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu inaipongeza wizara kwa kutekeleza maagizo yake kupitia Kamisheni ya Kukabiana na Maafa. Moja kati ya maagizo ya kamati kwa Wizara juu ya Taasisi hiyo ni suala zima la kuiongezea bajeti Taasisi ili iweze kutekeleza Majukumu yake kwa ufansi Zaidi. Agizo hilo limetekelezwa kwa karibia asilimia 43.5 ya bajeti ya 2017/18. Pia Kamati inaipongeza Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kuweza kufungua Akaunti Maalum kwa ajili kupokea michango ambayo Mhe. Waziri akaunti namba yake ameitaja.

Aidha Kamati inaipongeza Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa kwa kuweza kuwa na eneo la kuhifadhia vifaa vya maafa. Hata hivyo, Kamati yangu bado inasisitiza suala la kuwa na maghala ya kuhifadhi vifaa kwa Unguja na Pemba ni jambo la msingi na linalohitajiwa kupewa nafasi maalum ya utekelezaji.

Pia Kamati yangu inasisitiza suala zima la kuwa na maeneo maalum ya kuwahifadhi wahanga wakati wa maafa yanapotokea, Kamati imeliona suala hili ni muhimu sana na Kamati inataka wizara na taasisi husika ziongeze bidii kuhakikisha tunapata eneo kwa ajili ya kuwahifadhia wahanga wakati wa maafa.

Mhe. Mwenyekiti, Tume ya Ukimwi, Kamati yangu inaipongeza sana serikali Kwa kuwajali wananchi katika suala zima la kujali afya. Kamati yangu ilisisitiza suala la kuwa na Bima ya Afya kwa Wananchi. Kamati imefarajika sana kuona Serikali imeweza kutekeleza agizo lake hilo na kwa kuanza kuandaa Mswada wa Sheria ya Bima ya Afya. Aidha Kamati yangu inapongeza sana serikali kwa juhudi zinazochukuliwa na Serikali Kupitia Tume ya UKIMWI Zanzibar katika kutoa elimu kwa umma juu ya maradhi ya UKIMWI na madhara yake, vile vile kamati inapongeza kwa jitihada zinazochuliwa kuzisaidia taasisi ambazo zinajishirikisha na mapambano dhidi ya UKIMWI kwa kuzipatia mafunzo pamoja na kuziwezesha kuzipatia ruzuku ya fedha.

Aidha Kamati inapongeza juhudi za Tume ya Ukimwi katika kutafuta rasilimali kwa ajili ya utekelezaji wa muitiko wa *VVU* na UKIMWI nchini ikiwemo kupata wadau mbali mbali muhimu ambao wapo tayari kutoa mashirikiano ya kuendeleza mapambano dhidi ya maambukizi ya virusi vya Ukimwi.

Mhe. Mwenyekiti, Jumuiya ya Watu wanaoishi na *VVU (ZAPHA+)* ni miongoni mwa wadau wakubwa wa mapambano dhidi ya maradhi hayo. Kamati yangu inaipongeza sana serikali kwa kuweza kuisaidia jumuia hiyo pamoja na ukweli kwamba serikali inatoa msaada juu ya jumuiya hiyo. Lakini kamati yangu bado inaomba jumuiya hiyo ili iweze kusaidiwa angalau iweze

kumiliki jengo lile liliopo karibu na afisi hiyo. Jengo ambalo litatumika kama makau makuu za *ZAPHA+* kwa Zanzibar ili iweze kuratibu shughuli zao ambazo zinahusu maisha ya watu kwa kila siku wanaoishi na *VVU*.
Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ, Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu inapongeza juhudi ya za usimamizi na utoaji wa elimu wa miradi ya *TASAF III* za kwamba ni mpango endelevu wa utoaji wa elimu kwa walengwa na program hiyo ambao ni Kaya masikini. Kamati inasisitiza kuwa ni muhimu walengwa wa Progranmu hiyo kuendelea kuelimishwa kabla ya zoezi la uendeshaji wa miradi kuanza.
Mhe. Mwenyekiti, Hata hivyo, Kamati yangu imeelezea kutoridhika na hali ya Miradi ya *TASAF I* na II ambayo kwa asilimia kubwa ilikamilika lakini baada ya kukamilika baadhi ya miradi hiyo imetelekezwa na kutoendelezwa na taasisi zilizokabidhiwa miradi hiyo, ikiwemo miradi ya maji na miradi mingine mbali mbali iliyokusudiwa.
Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inazitaka wizara zote ambazo zilikabidhiwa miradi ya TASAF 1 NA TASAF II, zitambue kwamba zinawajibu wa kuendeleza na kuisimamia miradi hiyo ipasavyo ili iweze kutoa tija iliyokusudiwa.

Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ - DSM,

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu haina budi kuipongeza serikali kwa kuchukuwa jitihada za makusudi za kutaka kuboresha jengo la SMZ la Dar es salaam, dhamira ya serikali ya kujenga upya ni nzuri na yakupongezwa sana. Hata hivyo, suala pekee la kuliangalia kwa hivi sasa, ni kuhakikisha kwamba namna gani jengo hilo tunaendelea kulitunza vizuri ili lisijekuendelea kuharibika kabla ya kuanza kwa ujenzi huo.

Idara ya Watu wenye Ulemavu

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inaipongeza serikali kwa kutambua mchango wa watu wenye ulemavu kwa kuwaongezea fedha katika bajeti ya 2017/2018.

Aidha, kamati inaipongeza sana Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kuipatia gari moja na fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vingine vya kuimarisha utendaji kazi. Vile vile kamati inaipongeza wizara kupitia Idara ya Watu Wenye Ulemavu, kwa kuweza kuandaa dodoso la kubaini majengo ambayo hayana miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu. Kazi hiyo ni ya kupongezwa na ya kuungwa mkono, ili watu wenye mahitaji maalum nao waweze kuzifikia huduma hiyo kwa urahisi, pale wanapohitaji huduma hizo katika majengo mbali mbali ya serikali na taasisi nyengine za umma.

Aidha, kamati yangu inaipongeza Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, kwa kuhakikisha kuwa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto inaiwezesha Idara ya Watu Wenye Ulemavu, na kwamba inafanyakazi kwa ukaribu na watu wenye mahitaji maalum, kwa kuvipatia vikundi vidogo vidogo mikopo ili kuweza kujiendeleza katika shughuli zao za kiuchumi na ili kuweza kukimu maisha yao ya siku hadi siku. Ofisi hii imekuwa ikishirikiana na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto ili kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu wanapewa kipaumbele maalum katika huduma za mikopo zinazotolewa na wizara hiyo.

Tunaiomba Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto ambayo inatoa mikopo kwa vikundi vya ujasiriamali, ielekeze nguvu zake zaidi kwa watu wenye mahitaji maalum, ikizingatia kwamba hawa ni watu wenye umuhimu wa aina ya pekee ambao wanastahiki kupewa mikopo kutokana na hali za maumbile yao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa**,** kamati inaipongeza sana wizara kukubali ushauri wa kamati wa kuongeza Bajeti ya Idara hiyo, ili waweze kununua vifaa mbali vya kisasa ambavyo vitatumika katika sherehe za kitaifa.

Hitimisho:
Mhe. Mwenyekiti, baada ya maoni hayo ya kamati ambayo nimejaribu kuyaelezea, na yameweza kuelezea namna gani yameweza kuakisi kwa kiasi kikubwa hali ya utekelezaji katika Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, ni imani yangu kuwa taarifa hii ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa yatasaidia sana kuimarisha utendaji katika wizara hiyo. Kwa hivyo, nawaomba wajumbe wengine wa Baraza lako tukufu, waichangie vyema taarifa hii, kwa lengo la kupata utekelezaji bora na wenye maslahi yaliyotukuka kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa, napenda kukushukuru tena wewe binafsi, kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa ya kamati yangu kwa niaba ya kamati, pamoja na kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza vyema na kwa umakini mkubwa. Sasa niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, waijadili ili wamuwezeshe waziri kufanikisha kazi zake kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya kamati ninayoiongoza ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, naomba kutoa hoja. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mjumbe Mwenyekiti wa Kamati. Sasa niwaombe Waheshimiwa Wajumbe kwamba hizi taarifa zote zinataka kuchangiwa. Kwa hivyo, hadi sasa wachangiaji ni kidogo, kwa hivyo endeleeni kuleta majina yenu ili muweze kuchangia. Lakini muende moja kwa moja kwenye hoja iliyombele yetu katika kuchangia kwetu.

Waheshimiwa Wajumbe, jengine ni tangazo la wageni, wageni wetu wa leo tarehe 29/09/2017 ni wageni wa Mhe. Simai Mohammed Said Mpakabasi kutoka Jimbo la Tunguu. Wageni wenyewe idadi yao ni 10 kutoka Unguja Kaebona, ambao wameambatana na Mwenyekiti wa Tawi, Katibu na Katibu Mwenezi. Wageni wenyewe ni kama wafuatao.

1. Ndg. Khatib Ali Khamis Mwenyekiti.
2. Ndg. Ibrahim Haroun Rashid Katibu
3. Ndg. Ramadhani Mzee Ali Katibu Mwenezi
4. Ndg. Solbah A. Iddi Mwenyekiti wa Wazazi
5. Ndg. Mwatima K. Rajab Mwenyekiti UWT

Mhe. Mwenyekiti, wageni hao wameambatana na Wajumbe wa Kamati ya Siasa ambao ni:

1. Ndg. Rashid Haroun Rashid

2. Ndg. Mlekwa Mabele Kulwa
3. Ndg. Andrea Jonathan Sanaheri
4. Ndg. Saumu Julius Tame na
5. Ndg. Suleiman Rashid Ali Mjumbe wa Halimashauri.

Nasema karibuni katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, tangazo jengine ni kutoka kwa Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto Zanzibar Mhe. Maudline Castico, anawatangazia kwamba wajumbe wote wa Baraza kwamba kutakuwa na siku ya wazee duniani, itakuwa siku ya tarehe 01/10/2017. Tunaombwa kualika na kuhudhuria kwa wingi katika Chuo cha Chwaka na mgeni rasmi atakuwa ni Mhe. Balozi Seif Ali Iddi Mhe Makamu wa Pili wa Rais. Tunaombwa kuhudhuria, hiyo ni siku ya wazee lakini na vijana wanapaswa kwenda kushereheka na wazee wao. Baada ya hayo tunaendelea. Waheshimiwa Wajumbe, mchangiaji wetu wa mwanzo ni Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa na kuweza kuichangia Taarifa ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka wa fedha 2016/2017

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikupongeze kwa kunipa nafasi hii ya mtu wa kwanza baada ya Mwenyekiti. Lakini pili nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kazi nzuri ya taarifa hii ya kupewa maagizo na kuyajibu ili kutupa mwelekeo mzuri katika utekelezaji wa kazi zao.

Lakini pili, niipongeze kamati chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Omar Seif Abeid na wajumbe wake wote kwa kazi nzuri ya kuipa maagizo wizara mbali mbali na kutupa maelekezo mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza nitasema machache kabisa. Mhe. Mwenyekiti, naiomba tu wizara iongeze bidii juu ya ufanikishaji wa kazi zake. Kwa bahati nzuri Mhe. Mwenyekiti, katika kukisoma kitabu hiki, taarifa ziko nyingi na nzuri, lakini pia zina changamoto ambazo zimejitokeza, inafaa kupongezwa na kupewa ushauri.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 2, Tume ya Kitaifa ya Utaratibu wa Udhibiti wa Dawa za Kulevya. Mhe. Mwenyekiti, katika nchi yetu tunaelewa kwamba hili ni janga la kitaifa na janga hili ni sawa sawa na vita katika nchi Mwenyezi Mungu atuepushie, visitokee vita vya silaa kati ya nchi yetu na watu wengine wowote wabaya. Lakini hili la dawa za kulevya ni vita vigumu sana, hasa tukizingatia kwamba vijana wetu wengi wameathirika, wanapotea na hawajielewi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa kamati iliiomba wizara kuongeza bajeti katika fungu lake na kuweza kuongezewa pesa ambazo ni kama shilingi 159 milioni ambazo ni nyongeza katika bajeti ya mwaka 2016/2017, ambayo ilikuwa ni shilingi milioni 339,900,000/- na kufikia shilingi milioni 598,900,000/- kwa mwaka 2017/2018, ni ongezeko la fedha ambazo ni milioni 159. Mimi naipongeza sana wizara na naipongeza kwa dhati kabisa kwa kujua kwamba hili ni tatizo ambalo linatuathiri kwa vijana wetu ambao wanapotea.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitowe mfano. Katika kufuatilia mambo mbali mbali na kudhibiti dawa za kulevya katika Jimbo langu la Kijitoupele, nitaseme upande wangu na mengineyo, lakini nitasemea upande wangu zaidi. Eneo langu la Shehia ya Tomondo au Uzi huko kuna maafa makubwa ya dawa za kulevya, na hii inatokana na vijana wetu ambao wamewekewa ulinzi mkali katika sehemu mbali mbali, kama Miembeni, Mikunguni na sehemu mbali mbali za mjini, sasa imekuwa makimbilio yao yamekuwa ni kule.

Kwa hivyo, naiomba sana wizara kwa kupitia vyombo vinavyohusika lifuatiliwe hili ili kuwanusuri wananchi wangu wa maeneo hayo. Hilo eneo naweza kulisema kwa jina ambalo sio kama ndio jina lao au ndio watumiaji, linaitwa Kwa Walevi. Mhe. Mwenyekiti, hilo jina ni la umaarufu tu. Kama vile mimi naitwa Shihata sio baba yangu, lakini umaarufu wangu ni Shihata tu. Kwa hivyo, na hilo eneo linaitwa Kwa Walevi naomba lifuatiliwe ili wananchi wetu wawe katika manusura. Wananchi wanapigwa visu ovyo, wanaibiwa na kuna majumba mabovu hayo ndio kimbilio la watu wanaotoka Miembeni na sehemu nyengine za mjini, kwa sababu mkakati umekuwa mkubwa kwa hivyo wanakimbilia huko. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naomba sana na naipongeza serikali kwa kuliona hili, lakini fedha zilizoongezwa zifanye kazi kwa kunusuru wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine baada ya kutoka ukurasa huu nitakwenda katika ukurasa wa 7, kuhusu Tume ya Uchaguzi. Tume ya Uchaguzi Mhe. Mwenyekiti, tukitaka tusitake ndio roho ya nchi hii, kwa sababu Tume inatakiwa kuwa na maeneo mazuri yenye usalama zaidi na yenye hifadhi ambayo itakwenda vizuri katika kufanyakazi zake na shughuli zake ziende vizuri. Mimi naipongeza serikali na pia nawapongeza na watendaji wote wa Tume ya Uchaguzi kwa moyo wao wa ujasiri na kufanyakazi zao vizuri.

Kwa hivyo, lile eneo ambalo Mheshimiwa katueleza kwamba baada ya kuombwa na kamati kwamba tunataka hiyo nyumba iliyokuwepo jirani inunuliwe ili kuipa nguvu tume kufanyakazi zake vizuri, kwa hivyo naiomba sana wizara suala hili lisichukuliwe muda, kwa sababu tume inataka kuwa huru na inataka kuwa katika mazingira yake peke yake ndio utaweza kuudhibiti ulinzi wa eneo lile. Kwa hivyo, naipongeza sana wizara kwa kuliona hili.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 13 kuhusu Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa. Mhe. Mwenyekiti, tunaambiwa kwamba katika maisha na ndivyo ilivyo hakuna bajeti ya maafa, ukasema kwamba nitapata maafa naweka hivi. Lakini unaweza ukaweka kima likitokea, sio dhamira kwamba litokee Mwenyezi Mungu atuepushie, lakini naipongeza serikali kwa kuona kwamba yanatokea majanga mbali mbali. Katika majanga ya maafa Mhe. Mwenyekiti, kuna maafa ya aina nyingi, sisi tumezungukwa na bahari, hivyo tunataka vyombo vya baharini vya uokozi, tunatumia ndege tuwe karibu katika mambo ya uokozi katika mambo ya anga. Pia tuna usafiri wa ardhini wa magari na kadhalika ndio usafiri wetu mkubwa basi tuwe karibu kupata vifaa vya kufukuzia. Vile vile kuna mambo yanaweza kutokea ya upepo na mvua.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi naipongeza serikali baada ya kupata agizo la kuongeza fedha za maafa kwa mwaka 2016/2017 na serikali ilichangia shilingi bilioni 850 na kufikia shilingi laki 867, mheshimiwa nafikiri hili lilikuwa kwa mwaka huo. Lakini kutokana na kuliona hilo serikali kutoka hapo ikaongeza fedha zake nyingi zaidi hadi kufikia shilingi bilioni

1,506,233,000 naipongeza serikali kwa kujua kwamba hili suala hatutegemei litokee, lakini dharura ni jambo la msingi kuweka akiba. Tumuomba Mwenyezi Mungu atuepushie lisitokee katika nchi yetu, lakini naipongeza serikali kwa hili kwamba madhali limewekwa litatusaidia.

Mhe. Mwenyekiti, tuna matatizo mengi katika majimbo yetu, nikisema nalia kwenye jimbo langu pia na majimbo ya majirani zangu ninao. Lipo Jimbo la Mwanakwerekwe tupo mpaka mmoja na Mhe. Abdalla Ali Kombo. Kwangu katika Jimbo la Kijitoupele hasa nalilia hili Ziwa Maboga ambalo tuko jirani na Jimbo la Chukwani, lakini maji yanayotoka Mwanakwerekwe, maji haya yanaelekea katika jimbo letu ambalo linaanzia Daraja la Shunda, hili ni daraja ambalo linachukua maji mengi na wananchi wake wanaathirika mwaka hadi mwaka. Kwa hivyo, naiomba Kamisheni ifuatilie na ijuwe uwezo wake zaidi ifanye nini ili itusaidie.

Nafikiri Mhe. Mwenyekiti, kama wizara itafuatilia kutokana na Kamisheni yetu hii, ili ikajua ile miundombinu iliyokuwepo na kuweza kuishauri serikali au ikashauri mambo mengine mazuri ya kuondolewa kadhia ile iliyokuwepo ya misingi ambayo haifai kwa wakati tuliokuwa nao na kujengwa misingi mipya. Kwa hivyo, naipongeza serikali kwa kuliona hili.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nitalizungumzia kidogo ni Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMT. Hii ni idara muhimu Mhe. Mwenyekiti, na idara hii tunahusiana nayo zaidi kwenye mambo ya Muungano. Kuna mradi wa TASAF, mradi huu ni mkombozi wa wanyonge. Lakini mradi huu tukikaa tunaufuatilia sisi wengine, tukiuangalia Tanzania Bara unawafikia walengwa maskini. Hapa kwetu, namuomba sana Mhe. Waziri anisikilize. Mhe. Mwenyekiti, tunapozungumza tunawaomba Waheshimiwa Mawaziri watusikilize, kwa sababu tunaizungumzia wizara yake mtu, wengine wacha wazungumze.

Mhe. Mwenyekiti, suala la TASAF, Tanzania Bara kama utaangalia kwenye vijiji mbali mbali vya watu maskini basi TASAF inawasaidia wanyonge. Mnyonge anakuambia tu, mimi nimepata kujenga banda langu hili hapa, nimepata kufuga kuku, nimenunua mbuzi na nimenunua ng'ombe maisha yake yanakwenda. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kwetu sisi kuna tofauti kidogo.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri kwa kupitia watendaji wetu, kupitia Masheha wetu wafanye uratibu tena wa kufuatilia ukweli, kuna baadhi ya wanyonge hasa hawaupati mradi huu, tena ndio wengi hawapati katika sehemu zetu. Mimi katika jimbo langu hawapati, kuna watu vijana kabisa wana uwezo na wanajinata hasa, aa! waache wahangaike tu lakini sisi tunapata. Mhe. Mwenyekiti, wapo tena mimi nipo tayari kutoa ushahidi na kuweza kuisaidia TASAF hii ili tufanye kazi na kuweza kuwanufaisha wanyonge ambao wana shida za kila siku. Suala hili Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri aliangalie na alichukuwe.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, kuna mambo mengine ambayo yanahusu Idara ya Watu Wenye Ulemavu. Mhe. Mwenyekiti, naipongeza serikali kwa kuliona hili, wenzetu hawa wanataka msaada wa aina mbali mbali na hasa tukizingatia kwamba sisi tuliokuwepo hapa ndio wadau wao namba moja, na sisi ndio tutakaowasemea katika shida zao. Kwa hili niipongeze wizara kwa kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwamba wenzetu hawa waangaliwe na wapewe uwezo.

Lakini niipongeze Wizara yangu ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kwa kuona kuna haja. Mimi katika kamati mara nyingi husema kwamba mnapotupa *data* zenu

Wizara yangu ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto basi tuambieni tu kwamba vikundi vya akina baba, kina mama na vijana wamepata mikopo, je wenzetu wenye mahitaji maalum wamepata nini. Kwa hivyo, naiomba sana wizara washirikiane sana na Wizara yangu ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, ili kuhakikisha kwamba wazee au vijana wetu hawa watu wenye mahitaji maalum ya ulemavu wanapata msaada huu wa mikopo midogo midogo na tuwasaidie kwa hali na mali.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa nampongeza sana Mhe. Waziri kwa kuangalia kwamba haya yanayozungumzwa au yaliyoletwa na Kamati yanajibiwa na naamini ndio muelekeo wa Wizara zote, hii itakuwa ndio Wizara ambayo imetoa muongozo na nyengine zinafuata kama ilivyo kwa sababu taratibu tunazijua, tunayoyachangia hapa ni kuisaidia Wizara na wanayotoa wenzetu kamati ni kuisaidia Wizara. Kwa hivyo nasema tu mimi kwa furaha kabisa naiunga mkono kwa asilimia mia moja taarifa hii ya utekelezaji kwa mwaka 2017/2018 tunakoendea. Ahsante Mheshimiwa nashukuru.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote ninze kwanza kwa kutanguliza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza leo kufika sote hapa kuwa wazima wa afya, lakini pia nikushukuru wewe Mwenyekiti kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia mawazo yangu, fikra zangu juu ya ripoti hii ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais juu ya taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya kusimamia Afisi za viongozi wakuu wa kitaifa ya mwaka wa fedha 2016/17.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru pia kwa utambulisho mzuri kabisa juu ya wananchi au viongozi wetu wa Chama cha Mapinduzi katika kijiji cha Unguja Ukuu Kaebona ambao leo wamekuwa wageni wetu hapa, nawakaribisha sana na sisi pia wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuendelee kuwapa moyo na tuzidi kuwaalika wengine na wengine katika kipindi hichi ambacho tunaendelea na uchaguzi wetu katika maeneo tofauti.

Lakini pia kabla sijaanza mchango wangu nichukue nafasi hii pia kumpongeza aliyekuwa Mkuu wetu wa Mkoa wa Kusini kwa uteuzi mpya ambapo kwa sasa atakuwa yupo rasmi chini ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais akiwa kama Katibu Mkuu, niseme tu Mkuu wetu tulikuwa tunampenda na sasa atakuwa Serikalini kwa hivyo tutazidi kuwa nae kushirikiana nae kwa karibu kutokana na kwamba Ofisi ya Makamo wa pili wa Rais inasimamia mambo mengi. Kwa hivyo hatokuwa mbali na mimi nikiwa Muwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Tunguu basi tutaendelea kushirikiana namtakia kila la kheri katika nafasi yake mpya ya kazi.

Mhe. Mwenyekiti mimi nitakwenda moja kwa moja kwenye madawa ya kulevya kwanza niipongeze sana Serikali katika juhudi za kuimarisha mambo yote juu ya kuhamasisha wananchi na vijana wetu ili kuepukana na janga hili, karibuni hizi kete zimeanza kupanda bei kete sasa imetoka shilingi 2000 aina ya *heron* mara hufika kwenye shilingi elfu 10 mpaka 15. Nasema hivi kwa sababu wakati

tunaondoa tatizo la madawa ya kulevya basi mengine hujitokeza hii ni *common* katika biashara *demand and supply* wakipungua bei inapanda, sasa tuzidi kuimarisha katika kupambana na janga hili na naunga mkono juu ya uwekwaji wa mabango katika maeneo hasa *point of entry* ambazo zinatakuwa ni ya bandari pamoja na *Air Port,* na kutangaza pia ile sheria jinsi inavyoweza kumfanyia mtu kama mtu atakosea na atatumia madawa basi ajue amekiuka sheria za nchi na hatua zinaweza kuchukuliwa. Hili pia linasaidia katika wageni ambao hutembelea katika visiwa vyetu kwa ajili ya kutalii na mambo mengineyo.
Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nataka nichangie kidogo kwenye suala la wakala wa Serikali wa uchapaji, vyombo tulivyokuwa tunavyo kwa wakala wetu ni vipya, vizuri, vya kisasa na inawezekana katika Jamhuri yetu ya Tanzania hakuna mtu au kampuni yenye mashine kama zile kwa vifaa tulivyokuwa navyo sisi, lakini bado matumizi yake na utaalamu wake unahitajika ili kuimarisha pia kupata biashara lakini pia kuwaunganisha kwa ukubwa zaidi taasisi pamoja na mamlaka tofauti za Serikali. Changamoto iliyokuwepo tumezisikia zilivyozungumzwa nataka nishauri vitu viwili mpaka vitatu.

Kwanza Kuitangaza Wakala wenyewe kuifanyia matangazo juu ya kazi zao kwa kutumia vyombo vyetu vya ndani vya habari, lakini pia vile vyombo pia kutumia mitandao ya kijamii.
Pili wawe na mpiga picha wa kwao wenyewe mpiga picha ambae atakuwa anatembea maeneo ya Zanzibar ili kutengezea *Library* yao, hili linasaidia pale ambapo kama unahitaji kutengeneza kalenda, unahitaji kutengeneza ripoti yako ya jimbo, unahitaji kuifayia ile manjonjo ili ipendeze. Kwa hivyo unapotaka ripoti yako ipendeze utahitaji picha za ziada ambazo wewe unakuwa huna na pengine huwezi kuzipata, sasa lazima wao wawe wana *Inhouse Photography* au mpiga picha ili ambae atapendekezesha majarida mbali mbali ya Serikali pamoja na taasisi za watu binafsi na hawa ma-*designer* wanaokuwepo ukiwaunganisha na hawa wapiga picha.

Kwa sababu hawa vijana wetu watundu watundu wapo wengi sasa hivi ambao ni ma-*Graphic Designer* wanaweza kusaidia sana na hakuna kampuni inayopiga chapa au *Printing Company* Duniani iliyoweza kuchukua hatua yoyote kama huna ma-*Designer* wa *Inhouse Designer* wazuri wa kuweza kupamba na kutengeneza vitu tofauti.

Lakini pia ningeshauri pia hawa ambao wanaajiriwa katika Ofisi yetu hii ya Serikali basi wapatiwe *Training* aidha katika nchi za ulaya lakini pia waende China, itakuwa ni ghali huko basi wapelekwe India wakienda India watajifunza

mengi sana na watakaporudi hapa tutaweza hata sisi kuwa katika wakala bora katika Afrika ya Mashariki na Kati.
Lakini nataka niseme kitu changine wamekuwa sasa wana-*prints* magazeti ya Zanzibar leo. Mhe. Mwenyekiti, gazeti la Zanzibar leo ni gazeti ambalo linatoa taarifa nyingi za Serikali, lakini gazeti la Zanzibar leo ukishamaliza kuli-*print* jioni halifiki Dar es Salaam kwa sababu magazeti ya Dar es Salaam yaaondoka Alfajiri saa 10 au 11 yanaondoka kuelekea Mikoani, baadhi ya *time* sisi Zanzibar tunamaliza ku-*print* hapa usiku hakuna usafiri wa kuweza kuyafikisha Dar es Salaam.

Sasa nashauri kitu kimoja wakala anaye- print gazeti la Zanzibar leo washirikiane na wakala yule ambae yuko Dar es salaam lile lile gazeti la Zanzibar leo nusu liwe *printed* hapa na liwe *printed* Dar es Salaam ili yale ambayo yanatakiwa yaende Mikoani yaweze kufikia kwa wateja wetu mpaka maeneo ya kanda ya Ziwa, Kagera, Kigoma, Rukwa, Ruvuma na maeneo yote ya Mikoani tofauti na Dar es Salaam. Kwa nini nasema hivyo hata matangazo yao katika gazeti la Zanzibar leo yataanza kupungua kwa sababu yale magazeti hayafiki kwa sasa hivi Dar es Salaam hata zile tenda ambazo wanatangaza Serikali watu wanakosa Dar es Salaam, juzi magazeti ya Zanzibar leo yaliadimika Zanzibar kwa sababu orodha ya wanafunzi wote wanaoomba kazi *Air Port* magazeti yakaadimika hapakuwa na Zanzibar leo hapa Zanzibar ina maana *demand* ipo watu wanataka kuyasoma lakini leo nimekwenda kutembelea ofisi yao unanunua magazeti kwa kilo yamekaa ndani. Leo ni aibu kuona gazeti la Zanzibar leo linakwenda kuuzwa likafungiwe maandazi gazeti lenye taarifa kubwa, waandishi wetu mahodari wameyafanyia kazi. Kwa hivyo njia iliyokuwepo ikiwa itakuwa *printed* and Zanzibar basi lazima tuweze kuya-*print* na Tanzania Bara.

Lakini pia tuhakikishe usalama wa taarifa za Serikali zinachapishwa katika ofisi hii ni nyeti ziwe zina usalama wake, kamera ziwe *monitor* ndani ya Ofisi na kila kitu kinachotoka kuweko buku maalum la kuandika la kujaza kutoka mlangoni na kila *box* linalotoka lipekuliwe vya kutosha na ikiwezekana kwa wale wafanyakazi ambao ni *junior* wameajiriwa wanapotoka waangaliwe wanachotoka nacho. Taafira za Serikali ni muhimu sana zisije zikatoka nje kabla ya wakati hasa bajeti zetu, hotuba za Rais pamoja na mengineyo.

Sasa naingia katika suala la maafa Mhe. Mwenyekiti, niseme nimesikitika sana leo katika ripoti ya Waziri jambo langu moja tu basi na katika Waziri ambaye ni makini sana ni Mhe. Mohammed Aboud Mohammed nampongeza sana kwanza kwa utaratibu wake lakini kitu kimoja kikubwa alichokuwanacho ni sifa ya kipekee jinsi anavyozungumza na watu na anavyotuheshimu Wajumbe wa Baraza la

Wawakilishi hasa *beck bencher* anaongea kwa unyenyekevu, anaongeza ili tumsikilize hatushambulii, hatutolei ukali tunajua kabisa kwamba anatujali.

Sasa leo nimpe masikitika yangu moja katika hotuba yangu hapa ya kuchangia bajeti kuu ya Serikali nilishauri juu ya nambari ya kupatikana ya maafa ili wananchi na Wazanzibari wote wapelekewe *message*, vimbunga vinapotokea na upepo mkali mimi jimboni kwangu Unguja Ukuu kwenye kisiwa cha Uzi, Bungi, Kikungwi kote ni wavuvi unapotokea upepo mkali wakati mwengine hawana taarifa kwenye redio wanazozipata lakini wote wana simu. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina sheya katika kampuni ya simu ya Zantel kuna tatizo gani Wazanzibari kupokea *message* juu ya hali ya hewa wakapata bure, tunapokea kila siku pokea huduma hii *message* fulani juu ya ofa lakini Mzanzibari, juzi kulikuwa kuna upepo mkali sana ulipiga hapo kama wiki moja nyuma kutoka Mkoa wa Kusini wakati Kusi anaendelea kumalizia huku.

Lakini upepo ule kwa wavuvi wetu wanaweza kupata taarifa mapema wanapata kujupanga hata mvuvi anapotaka kwenda baharini basi mke wake anaweza kumwambia mume wangu leo baharini usiende nimepata taarifa kuna upepo mkali, amimi nakwenda usiende mimi nakuzuia kaa ndani sasa hili ni muhimu, kwanza halina gharama halihitaji ubunifu linahitaji utekelezaji. Kwa hivyo nimuombe Mhe. Waziri pamoja na Ofisi yake watendaji wote na wananisikia kwamba naomba sana kwa mamlaka ya hali ya hewa inapotangaza juu ya vimbunga upepo utakaopiga ndani ya visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na ukanda wote wa bahari ya pwani taarifa itoke kwa kupitia *message* tutumie kampuni yetu ya simu ya *ZANTEL* na wananchi wote iwafike na chini iandikwe kutoka Ofisi ya Mamlaka ya Maafa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais.

Lakini pia niwapongeze pia juu ya bajeti mara hii nimeona bajeti imeongezeka kwenye kwenye milioni 655 nawapongeza sana Wizara ya Fedha, nashauri hivi vifaa ambavyo vimewekwa vya uokozi katika maeneo tofauti au katika historia walizoweka nimesikia juu ya masuala ya *Storage* yao Maruhubi, vitu vyote vifanyiwe *inventory* vihisabiwe kuwe kuna buku rasmi la kutambulika. Lakini pia *Account* waliyofungua PBZ isiwe na *Account* moja afungue *Account* katika Benk ya *NMB*, afungue *Account* katika Benk ya *Barclay* kote kuwe kuna *Account* za maafa mtu anapotaka kufanya *Transfer* iende moja kwa moja kama mimi nina *account* ya *Barclay* nikifanya *Transfer* leo inakwenda kwa nusu saa, lakini nikitoa benki moja kwenda kwenye benki nyengine muda wa kufika unachukua mrefu zaidi na pale ambapo tuna maafu tunahitaji utekelezaji wa shughuli zote kwa pamoja.

Lakini pia kwa upande wa Benki nashauri sana tufungue mtandao rasmi wa Zanzibar juu ya masuala ya *disaster* kwa sababu tuna marafiki wengi nje ya Zanzibar, tuna Watanzania wengi nje ya Zanzibar tuna Wazanzibari wengi ndugu zetu Arabuni na nchi za ulaya na hao wote fikiria akiamua kuchangia *Pound 5, Dollar 5 Euro 5* lakini lazima afanye *Internet Banking* anaingia kwenye *Web Site* anajaza kifomu chake kitu cha dakika mbili. Kwa hivyo watu wana hamu ya kufanya haya matendo lakini jinsi ya kutufikia haipo na mimi nipo tayari Mhe. Waziri ukitaka nikusaidie jinsi ya kufanya hili nitashirikiana na wewe pamoja na Mhe. Naibu Waziri ambae yuko makini ili tuweze kulifanya hili na likawa pamoja kabla ya mwisho wa mwaka haujesha.

Lakini katika hizi *account* tuhakikishe kwamba fedha zinazoingia mnazikamata vizuri sio matumizi yake yanakwenda katika maeneo mengine, yule ambae ananuiya duniani au yuko kokote kama yuko India, China, Marekani, Norway, Sweden anaamua kuwachangia Wazanzibari wenzake basi zile fedha zitumike kama alichokisema na ripoti iweze kutoka kwamba tumeyafanya haya na haya.

Sasa nataka niongelee kuhusu suala Ofisi ya Utaribu wa Shughuli za SMZ Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa mjumbe wa kamati inayoshughulikia masuala ya Afisi za Viongozi wa kitaifa kabla Mhe. Spika, kutangaza kamati yake ya bajeti na kunihamishia kule, nataka nimpongeze Mkurugenzi ambae anasimamia ofisi hii ya utaribu kwa shughuli za SMZ kule Dar es Salaam kwamba sasa tunaanza kuona mabadiliko juu ya ripoti na nimpongeze Mhe. Waziri. Kitu ambacho nimefurahia sana mchango wangu nilioutoa wakati wa bajeti umeanza sasa kufanyiwa kazi nampongeza sana kwamba sasa wametembelea balozi za Algeria, Cuba pamoja na kujenga masula ya Diplomasia kutumiwa Afisi hii ya uratibu masuala ya SMZ kwa upande wa Dar es Salaam.

Lakini moja ambalo utekelezaji wake bado haujaanza Mawaziri na Wizara husika wazidi kutumia maafisa katika Ofisi hii ya utaribu inapokwenda Dar es Salaam ili kuwekwa kwa ukaribu, pia pale ambapo wanapata mialiko kwenda katika balozi tofauti kwa ajili ya shughuli kama *National days* au shughuli ambazo za kawaida basi wahakikishe wanawasiliana na Afisi ya Uratibu wa masuala haya ya SMZ Dar es Salaam ili waweze kuwakilisha. Lakini pia najua wataanza kufanya *training* wale watumishi walioko Dar es Salaam kwenda Kongo hili jambo ambalo nalipongeza sana kuwa wataendelea kujifunza Diplomasia na nazidi kusisitiza kwamba waendelee kujifunza lugha za Kichina pamoja na lugha ya Kifaransa wawe karibu na ikiwezekana pia lugha ya Kiarabu kwa fursa zote ambazo zitatokezea wanaposhirikiana pamoja na Afisi ya Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano Dar es Salaam mama yetu mama Samia Suluhu Hassan, basi yale yote

ambayo tunashirikiana kwa pamoja yawe yanakwenda vizuri pamoja na Wizara zetu.

Nasisitiza Mawaziri waendelee kuitumia Ofisi hii ili zile kazi zao ziweze kufanyika, na pale ambapo wanapokea mialiko ya semina au mikutano kama hawawezi kufika basi uwakilishi wao uwepo kwa kupitia ofisi hii. Lakini pia nashauri wafanye vipindi vingi visiwe kwenye SMZ lakini pia mafanikio yao pia watumie Televisheni ya *TBC, ITV, Azam* na nyenginezo ili kuimarisha muungano wetu na yale ambayo wanayafanya.

Suala jengine nataka nimalizie juu ya Idara ya Watu wenye Ulemavu Mhe. Waziri nimeona kwamba bajeti kidogo kuna maendeleo lakini niseme bado haitoshi, nikuombe sana tutumie ubunifu wa ziada kwa marafiki zetu tuzidi kuwaunganisha na nchi tofauti kwa yale yote ambayo wameyakusudia, na nikuombe Mhe. Waziri kama itawezekana katika kuweka usawa na kuwafanya hawa wenzetu wenye ulemavu kuwa karibu basi utuombee mechi ya mpira baina ya timu yetu ya Baraza la Wawakilishi pamoja na watu wenye masuala ya ulemavu, uwanja wa Amaan Usiku ili tuweze kufanya michango, tusherekee kwa pamoja sote Wazanzibari wengi wajitokeze na tucheze nao kwa pamoja na ikiwezekana mgeni rasmi tutafute kiongozi wetu mmoja wa kitaifa aje kutuunga sisi mkono.

La mwisho nichangia idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa Mhe. Waziri sherehe za Mapinduzi mwaka huu zilikuwa za aina yake kwa kweli mnastahili pongezi sana, watu walikuwa wengi ile haikuwa sherehe unaweza kusema ilikuwa ni tamasha tena tamasha kubwa watu walitoka maeneo tofauti hasa pale Mnazi Mmoja kuangalia vikundi na mambo mengine pamoja na usiku ule kuonyesha masuala ya fash fash, niseme tu kwamba tujitahidi mwaka huu wingi wa watu waliojitokeza mwaka huu kuelekea mwaka ujao 2018 basi *ZECO* waimarishe masuala ya taa barabarani kwa kushirikiana na Manispaa yetu hasa kwa upande unaoelekea Mnazi Mmoja na upande wa juu unapotokea Kilimani na njia ya kati inayoelekea Gymhana na magari yote yaweze kuishia kwa upande wa Baraza la Wawakilishi la zamani ili kulinda usalama wa watu na mali zao pamoja na mengineyo.

Lakini pia katika vile vikundi ambavyo vitakuwepo vya sanaa basi vitambulike na mapema ili wageni wetu wanaotaka kutoka Dar es Salaam kuja kushiriki katika Sherehe za Mapinduzi waweze kujipanga na mapema watambue ile ratiba jinsi gani tutakapokwenda pale Mnazi Mmoja, au Uwanja wa Maisara kwa ule mkesha wetu wa sherehe za Mapinduzi pamoja na yote yanayofanyika pale.

Mhe. Waziri nikupongeze juu ya suala la kuanza kununua vifaa ambavyo vifaa hivi pia vitandelea kutoa huduma kwa Wazanzibari viendelee kutangazwa katika kumbi tofauti wafaidike, pasiwe na faida kubwa sana juu ya jinsi gani vinavyokodishwa basi viwe kwa ajili ya manufaa ya Wazanzibari viweze kutumika hasa haya mashamiani, viti, meza na mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nichukua nafasi hii kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati na nikushukuru wewe pia kwa kunipa hii nafasi na wote ambao walioshiriki katika utekelezaji huwo wa ripoti hii na niseme kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Tunguu naunga mkono taarifa hii ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi juu ya kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa wa mwaka wa Fedha 2016/17 mia juu ya mia. Ahsante sana kwa kunisikiliza.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Simai Mohamed Said (Mpakabasi) Mwakilishi wa jimbo la Tunguu, sasa namwita Mheshimiwa wa Jimbo la Ziwani Mhe. Suleiman Makame Ali na baadaye atafuatia Mheshimiwa Mwakilishi wa Bububu Mhe. Masoud Abrahman Masoud.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangi taarifa ya utekeleza ya maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi inayosimamia Afisi za Viongozi Wakuu.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kutoa mchango wangu kwa heshima kubwa na kwa ruhusa yako naomba kutoa pongezi kwa Dkt. Idrisa Muslim Hijja aliyekuwa Mkuu wa Mkoa Kusini kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu Wizara hii ya Nchi, Afisi ya Rais, Makamo wa Pili wa Rais, mimi nimtakie kila la kheri na wale wote walioteuliwa hivi juzi kutekeleza majukumu yao ili kuhakikisha tunapiga hatua za maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, badala ya hapo niende kwenye ukurasa wa 7, inasema kama Kamati iliagiza serikali kuhusu masuala ya Afisi ya Tume ya Uchaguzi. Kamati ilitaka kwamba majengo ya Tume ya Uchaguzi yajengwe. Hata na mimi naunga mkono hilo kuhusu majengo. Kusema ukweli nchi inagh'ara kwa majengo. Lakini pia kila siku tunapiga kelele kuhusu suala hili la majengo tunavyoona kwamba serikali inakodi sana, fedha zile za maendeleo za kupeleka kwenye shughuli za maendeleo zinakwenda kwenye majengo. Naomba sana kwamba serikali kupitia Wizara hii kwenye jengo hayo ni kupewa kipa umbele kuhakikisha kwamba serikali inamiliki majengo yake wenyewe na kuacha kukodi ili kuhakikisha kwamba ile pesa tunayoipitisha kwenye Bajeti inakwenda kwenye maendeleo moja kwa moja.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye ukurasa wa 9 kwenye Tume ya Uchaguzi hapo hapo kwenye masuala ya magari. Suala hili la magari katika maofisi ya serikali magari siku nyengine unalikuta gari limepata pancha tu lakini inatiwa vichokoroni huko inafichwa anasubiriwa Mhe. Salma hapa atowe milioni mbili auziwe. Sasa hivi hatuwezi kufika, leo ukenda Tume ya Uchaguzi kuna magari, yaani karibu ofisi zote za serikali kuna magari siku nyengine ukiuliza gari unaambiwa umepata pancha, utashangaa kwamba sisi pesa hizi tunazczitaka kwa ajili ya kuendeleza nchi yetu kupiga hatua za kimaendeleo, leo tunatengeneza gari ile ile ambayo kwamba matengenezo yake ni madogo.

Mhe. Mwenyekiti, la kusikitisha zaidi ni kwamba hii kamati niiombe itie mkazo zaidi inapokwenda kule kuhakikisha, pindipo kama Wizara hapa imesema kwamba wamelifuatilia hilo na wamepeleka karakana yale magari kutengenezwa. Lakini na mimi niombe kwamba haya magari yaangaliwe kwanza na kuwe na mpango maalum wa kuhakikisha kwamba haya magari na vyombo vyengine vile vya mle maofisini visifichwe tu, chombo kikiharibika kitengenezwe. Sio kama leo mtu anakichukua chombo anakificha chombo kipya, kizima, kimepata pancha anataka kuuziwe mtu kwa lengo lake yeye mwenyewe, hatuwezi kufika Mhe. Mwenyekiti. Niyombe Kamati izidi kulisimamia hili na Kamati zote watakapokwenda kwenye Mawizara wakiliona hili wazidi kulisimamia na tulisemee na tulikemee.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye ukurasa wa 19 kuhusu masuala ya TASAF Kaya Masikini. Hapa Mhe. Waziri alisema kwamba tayari kwamba kuna wale waliokuwa hawafai kupewa zile pesa za Kaya Masikini wanaonufaika, tayari wameshaanza kuchukuliwa hatua. Lakini haiyonyeshi kwamba ni watu wangapi wamegundulikana na hawa watu wapo kila sehemu wanaopata pesa zile, wapo watu hawana sifa ya kupewa pesa zile lakini hapa idadi haikuonyesha kama mfano Chakechake ni wangapi au Wete au Mjini Magharib, haikuonyesha idadi.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba hapa tupate idadi sahihi ya kuweza kuwajua hawa watu ambao hawana haki ya kupewa pesa hizi lakini wananufaika na wanapata. Ingekuwa vizuri zaidi tungeorodheshewa kwamba hapa idadi fulani tayari wameshafukuzwa, tukajua kwamba kweli hii Kamati inafanya kazi. Lakini tukiambiwa tu kwamba tayari wameshaanza kufanya utafiti. Sasa utafiti huo kila siku utaauliza maswali humu Barazani lakini sasa ukifikiria kwamba majibu yatakuja hapa kuweza kujua angalau wangapi wameshachukuliwa hatua, majibu hayapo.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye suala la watu wenye ulemavu. Watu wenye ulemavu hapa imesemwa kuhusu masuala ya kupatiwa taaluma. Lakini Wizara ya Uwezeshaji tunaipitishia bajeti hapa kuhusu masuala ya Mikopo, Uwezeshaji Wananchi, Kiuchumi na Ushirika, masuala ya mikopo yale, lakini watu wenye ulemavu mara nyingi hawanufaiki na pesa hizi. Hata humu haionyeshi kwamba watu wenye ulemavu wangapi wa aina zote kwamba wamepata mikopo kiidadi, hamna kabisa imeonyesha tu kwamba tayari wamepatiwa taaluma. Taaluma nayo ni nzuri lakini vile vile angalau ule mtaji kuweza kujiwezesha wao wenyewao, lakini hiyo nayo pia haimo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi yangu yalikuwa ni hayo niiyombe zaidi Wizara pamoja na Kamati kusimamia na kutilia mkazo zaidi, kwa sababu ikiwa Kamati itakwenda tu pale kunywa maji na kuondoka kusema la ukweli hakuna litakalo fanyika. Nimuombe Mhe. Mwenyekiti wa Kamati, Mhe. Omar Seif bin Abeid, ahakikishe kwamba ofisi hizi za viongozi wakuu amezisimamia ipasavyo ili kuhakikisha kwamba ikiwa kama kuna matatizo au changamoto aziibue atuletee hapa ili kuhakikisha wananchi wote wanajua kwamba kweli Baraza la Wawakilishi wanafanya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naunga mkono lakini pia namuomba sana Mwenyekiti wa Kamati ahakikishe kwamba hayo mambo tuliyomueleza humu anayafanyia kazi na sisi tupo pamoja na yeye, tutashirikiana kwa hali yoyote. Ahsante sana.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana hapa tukiwa wazima na mimi nichukue fursa hii ya kuchangia taarifa ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa Mwaka wa Fedha 2016/17.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze moja kwa moja kwa kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kumteuwa ndugu Dkt. Idrissa kuwa Katibu Mkuu katika Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Pili nimshukuru Mhe. Waziri katika Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa kutekeleza vizuri maagizo ambayo yametolewa na Kamati katika taarifa zake.

Mhe. Mwenyekiti mimi niende moja kwa moja kwenye suala la madawa ya kulevya. Madawa ya kulevya sasa hivi kwa Zanzibar kidogo yamepungua kwani juhudi kubwa inafanyika katika ofisi hiyo. Pia niwapongeze Wakuu wetu wa Mikoa yetu yote ya Zanzibar kwa juhudi wanazozifanya ili kupunguza tatizo hili. Tatizo hili ni tatizo sugu kwa Zanzibar na sasa hivi linapoteza muelekeo wa vijana wetu kwa shughuli za maendeleo.

Nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi kwa juhudi kubwa ambayo sasa hivi anaichukua kwa kuhakikisha madawa ya kulevya katika Mkoa wake yanapungua lakini pia kuondoka kabisa. Madawa ya kulevya ndiyo yanayosababisha matatizo yote katika nchi yetu. Madawa ya kulevya sasa hivi mjini yameondoka na yanasogea vijijini, niwaombe Wakuu wa Mikoa wote waendelee kufanya juhudi pamoja na Wakuu wa Wilaya ili kuhakikisha kila eneo ambalo linasemekana kunauzwa madawa ya kulevya waweze kudhibiti.

Mhe. Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kuwapongeza wale Wajumbe wa Kamati ya ulinzi wa usalama kwa sababu kazi hiyo bila ya juhudi yao yasingeliondoka madawa, lakini wanajitahidi kufanya kazi na waendelee kufanya kazi na waondokane na kile kinachosema kuwa wanachukua vitu vidogo ili kuwaachia dawa za kulevya ziendelee kubakia. Naomba Mwenyezi Mungu awasaidie kufanya kazi ya uadilifu ili dawa za kulevya ziondoke Zanzibar ili wananchi wetu wapate kufanya shughuli zao za kimaendeleo wakiwa na nguvu na afya nzuri zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo niende moja kwa moja kwenye suala la Tume ya Uchaguzi. Niipongeze Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwanza kwa kuwatafutia kiwanja ambacho watajenga Ofisi za Tume ya Uchaguzi ili kupunguza ule msongamano ambao upo katika Makao Makuu ya Tume ya uchaguzi, unapokwenda na shughuli yako ya aina yoyote inabidi ukae foleni lakini kama kila Wilaya itakuwa na Ofisi yake naamini tatizo la msongamano kwenye Afisi Kuu litaondoka.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo nizungumzie lile suala la magari machakavu ambayo yapo katika Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, magari tunaambiwa yapo 11yakiwemo mengine Pemba na mengine Unguja. Magari yakiwa machakavu kweli yanakuwa yanaitia serikali. Niombe kamati ilipendekeza magari yakiwa machakavu sana yauzwe, lakini niombe kama alivyosema Mhe. Mwakilishi pale yakiwa ni mabovu kweli yauzwe ili yapatikane mapya. Naamini serikali huwa haitaki ununuzi wa magari yaliyokwisha kutumika, inatakiwa yanunuliwe magari mapya. Lakini nimeona zimeingizwa hapa shilingi milioni 200 kwa ununuzi wa magari mapya siyo

magari mengi unayoweza kupata kwa shilingi milioni 200. Niombe kama kunauwezekano magari haya ya kutengenezwa yatengenezwe ili kuwapunguzia tatizo la usafiri, lakini kama hayatengenezeki yauze ili hizi fedha milioni 200 ziweze kuongezeka yaongezewe magari mengi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo twende moja kwa moja kwenye suala la Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa. Imekuwa sasa hivi ni uzoefu kila inapofika kipindi cha masika inaonekana Zanzibar tunakuwa na matatizo. Niiyombe Serikali ya Mapinduzi Zanzibar hasa Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Manispaa pamoja na Halmashauri wafanye kazi ya kuhakikisha wale wanaojenga kwenye mabonde ya mpunga ambayo wananchi walitakiwa walime mpunga na mazao mengine, sasa kusijengwe nyumba za kuishi kwa sababu kila inapofikia kipindi cha masika serikali inajiandaa na kwenda kuokoa watu kutoka kwenye mabonde ya mpunga na kuwaeka kwenye skuli. Kwanza tunawanyima vijana wetu kwenda kupata elimu, lakini la pili serikali inapata hasara na inakuwa kwa wakati ule ni lazima tufikirie suala la kwenda kuwaondoa wenzetu mabondeni ili kubakisha eneo ambalo litakuwa salama. Niiombe serikali kwa kupitia Wakuu wa Mikoa na Wilaya na Wakurugenzi wasimamie huu ujenzi holela ambao unajengwa kenye mabonde baadaye yanatuletea athari.

Mhe. Mwenyekiti, ukizungumzia suala la ukimwi ni lazima uzungumzie na suala la masawa ya kulevya. Ukimwi Zanzibar sasa hivi ipo, haidhuru wataalamu sasa hivi wanatwambia unapungua. Kama madawa ya kulevya yatapungua na ukimwi nao utapungua. Niomba sana suala la elimu liendelee kutolewa kwa wananchi wetu. Elimu zaidi huwa inatolewa kwenye Televisheni, redio na magazeti. Niombe sana na Maafisa wa afya wa Wilaya wapewe kazi kwenda vijijini kuwaelimisha wananchi wetu ili waweze kuondokana na suala zima la ngono uzembe ili wasipate maradhi ya ukimwi sasa hivi imekuwa ni tishio kubwa kwenye visiwa vyetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo niende kwenye Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali hasa masuala ya TASAF. Niipongeze Serikali ya Jamhuri ya Muungano pamoja na Serikali ya Mapinguzi ya Zanzibar hasa kwa kusaidia zike kaya masikini. Wenzangu waliotangulia kusema walisema kuwa kuna baadhi ya maeneo au badhi ya Shehia walipopata agizo la kuandika watu wenye kaya masikini waliangaliana zaidi kifamilia. Kwa kuna watu wana uwezo wa kufanya kazi lakini wameingizwa kwenye kaya masikini, lakini kuna watu masikini zaidi hawakuingizwa kwenye kaya masikini.

Naomba huu uhakiki labda Mhe. Waziri atakapokuja atwambie baada ya uhakiki nini wamekigundua labda kwenye Wilaya fulani wamegundua watu waliokuwa hawana haki ya kupata huu msaada walikuwa 200 lakini sasa hivi wametolewa 20 wamebakia mia moja na ngapi tupate angalau muelekeo tuone kama kweli uhakiki umefanyika kuliko inavyojionyesha katika maandishi kuwa uhakiki umefanyika lakini hatukuonyesha kwamba uhakiki baada ya kufanyika nini kimepatikana.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia suala la miradi ambayo huwa inafanyika kwa mfano kuna baadhi ya maeneo wanasaidiwa suala la umwagiliaji na maeneo mengine. Kuna baadhi ya maeneo bado mpaka leo serikali ya Jamhuri ya Muungano imetoa fedha zake kwenye TASAF lakini mpaka leo mabonde mengine hayafanyi kazi. Kuna watu ilikuwa fedha zile wapewe ziwasaidie lakini zimetolewa halafu zimekwenda kukaa tu kunasubiriwa awamu nyengine ya TASAF ndiyo

ikapatikane awamu moja imepishwa mradi ulifanyika awamu imepishwa umekuja kwenye mradi mwengine. Niombe tu Waziri atakapokuja atuthibitishie kuwa hiyo hali ya miradi ambayo ipo hali kama hiyo tija yake inakuwa vipi.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo niende moja kwa moja kwenye suala la maadhimisho ya sherehe za kitaifa. Suala la maadhimisho ya sherehe za kitaifa ni nzuri na sote tunaipongeza serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa jinsi inavyothamini maadhimisho ya kitaifa hasa Sherehe za Mapinduzi. Hili kidogo naomba Mhe. Waziri atakapokuja atwambie kuwa unatumika utaratibu upi mpaka Mhe. Mwakilishi hapati kadi ya kwenda kwenye sherehe za Iddil Fitri, wala hapati kadi ya kwenda kwenye sherehe za Iddil Hajj, lakini unamkuta kijana tu Sharobaro basi anakadi tena anakwenda kukaa karibu na viongozi Wakubwa wa Kitaifa. Sijui kunakuwa na utaratibu gani zile kadi zinatolewa mpaka unakwenda kumkuta mtoto wa kawaida ana kadi kenda kukaa maeneo ambayo siyo mazuri kwa kukaa mtoto kama huyo.

Mwisho niseme tu kwamba naipongeza Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa jinsi walivyotuandalia utekelezaji wake. Lakini niombe tu kuwa utekelezaji huu ulioandikwa humu kama Mwenyekiti alivyotangulia kusema basi na utekelezaji wa kikweli ukaonekane kwenye maeneo ambayo kamati inakuwa inafatilia. Nimpongeze tu Mwenyekiti wa Kamati kwa jinsi alivyosoma hii taarifa kwa utulivu kabisa na kwa sababu yeye ndiyo Mwenyekiti naamini yaliyoandikwa humu yatakuwa ya ukweli yeye pamoja na Kamati yake imeyaridhisha.

Na sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na mimi naridhika kwa asilimia 100 naiyunga mkono.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Masoud anafuatiwa na Mhe. Mwantatu Mbarouk na mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi, ili tuweze kumpa Mhe. Waziri na yeye kujibu hoja za Wajumbe.

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa fursa hii na mimi kuweza kuchangia taarifa hii ambayo imewasilishwa mbele yetu. Nianze kwanza kwa kumpongeza Mhe. Waziri kwa kutuwasilishia taarifa hii ambayo imeeleza vyema utekeleza wa maagizo aliyopewa na Kamati.

Pili niipongeze serikali kwa hatua inayoichukua ya kuhakikisha linaandaa mikakati madhubiti ya kudhibiti usambazaji na utumiaji wa dawa za kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe tena fursa hii kuwapongeza askari wa kitengo cha dawa za kulevya pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi kwa juhudu kubwa wanazozichukua za kuhakikisha wanapambana na biashara za dawa za kulevya Zanzibar.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, jitihada zao zote zinagonga ukuta kutoka na kwamba wale watu watuhumiwa wa dawa za kulevya wanaokamatwa wanapofika katika vyombo vya sheria wanapewa dhamana na hii ni haki yao haki ya dhamana ipo kwa watuhumiwa wapo walionyimwa dhamana kisheria lakini wapo waliopewa dhamana kisheria.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, miye ningelishauri katika hili kutokana na uzito wa tatizo na changamoto kubwa inayoletwa na kwa wafanyabiashara pamoja na watumiaji wa dawa za kulevya, mimi ushauri wangu mkubwa ni kwamba sheria ya adhabu tuifanyie marekebisho tuifanyie marekebisho ili kuondoa dhamana kwa yoyote anayekamatwa na dawa za kulevya iwe kiwango kikubwa iwe kiwango kidogo kwa sababu tatizo hili kwetu ni kubwa yule ambaye anakamatwa na kiwango kidogo kile kikubwa kaweka ndani hatembei na kikubwa anatembea na kile kidogo anauza akisha anaenda kuchukua kidogo anauza akisha anachukuwa chengine kidogo. Kwa hiyo tukisema huyu ana kiwango kidogo tumepe labda dhamana au tumpe adhabu nyepesi huyo anakiwango kikubwa hatujaweza kuwapima hawa kwasababu wakijua mimi nikikamatwa na kiwango kidogo nitakuwa na tahfifu lakini wote tuwaweke katika kundi moja ambao wanafanya biashara hatarishi kwa lengo la kunusuru vizazi vyetu lakini pia kuliokowa taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, nije ukurasa na 13 ukurasa wa 13 kuna agizo la kamati linasema kwamba taasisi zenye madeni hufanya utaratibu wa haraka kulipa madeni yao ili kiwanda kiweze kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi. Kwa kuokoa muda sitaki kurejea nyuma naamini waheshimiwa wajumbe wazamelifuatilia hili ukurasa wa 13 *paragraph* ya mwanzo juu hilo ni agizo la kamati. Lakini imeelezwa kuwa katika utekelezaji tayari Serikali imetowa maelekezo kwa Wizara na Taasisi kulipa madeni hayo kupitia bajeti zao na baadhi ya Wizara na Taasisi zimeshaanza kulipa.

Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri atusaidie ni Wizara zipi kati ya hizi ambazo zimeanza kulipa madeni yao ni kwa asilimia ngapi ya madeni.

Mhe. Mwenyekiti, nije ukurasa wa 26 ukurusa wa 26 imeelezwa kwamba Idara ya Watu wenye Ulemavu imeandaa dodoso pamoja na ratiba ya ukaguzi wa majengo, lakini ukaguzi huu imeonyesha kwamba imefanyika kutoka 3/09/2017 umefanyika katika eneo ya Mjini Maghari tu Mkoa wa Mjini Magharibi ili kugundua majengo yasiyofikika.

Mhe. Mwenyekiti, nilitaka nipewe ufafanuzi na Mhe. Waziri kwanini ukaguzi huo uzingatie Mikoa yote kwasababu hayo majengo ya umma yanajengwa katika Mikoa yote na watu wenye ulemavu wamo katika maeneo yote hasa ukizingatia vijijini kuna majengo ya maskuli ambayo yanajengwa watoto wenye ulemavu watahitaji kupata elimu endapo jengo litajengwa katika mazingira yaliyokuwa sio rafiki hawatoweza kupata elimu lakini vile vile majengo ya Serikali watu wenye Ulemavu wanahitaji kupata fursa kushiriki katika majengo yale mfano ya Serikali kwa lengo la kupata huduma ambazo wanazihitaji na endapo yatajengwa yakiwa sio rafiki wanashindwa kutumia majengo haya. Kwa hiyo Mhe. Mwenyekiti niombe kwamba huu ukaguzi wa ugunduzi wa majengo yasiokuwa rafiki ufanyike kwa Mikoa yote ili kuona ukubwa wa tatizo liliopo na kama walivyoeleza katika taarifa hii kwamba wanataka kuchukua zile hatua za makusudi kuhakikisha suala hili linakaa vizuri.

Lakini mwisho nimpongeze sana Mhe. Waziri kama nilivyoanza kumpongeza lakini nimuombe azidi kusimamia hasa Idara ya Watu Wenye Ulemavu tuone kwamba watu wenye ulemavu wanafaidika na haki pamoja na fursa zilizomo katika nchi yao, kwasababu mara nyingi huwa kuna malalamiko wanakosa fursa wanakosa haki lakini nimuombe Mhe. Waziri kwa ninavyomuelewa juu ya uwelewa wake na kuumwa kwake na kuguswa na haki za Watu Wenye

Ulemavu pamoja na watu wenye ulemavu azidi kulisimamie suala hili ili watu watu wenye ulemavu waweze kufaidi fursa zilizopo, ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mwantatu mchangiaji wetu wa mwisho ni Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi tafadhali karibu sana.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa fursa hii ya kuchangia katika mada hii nzuri kabisa iliyowasilishwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais.

Kwanza kabisa naipongeza sana hotuba hii imewasilishwa vizuri walioulizwa maswali wameuliza vizuri sana na waamejibiwa vizuri maana yake mpaka vifungu vya sheria vinavyohusina na utekelezaji wa hayo yaliyoulizwa basi pia vimekuwa quo*te up*.

Kwa kuanza na mimi niungane na wenzangu kupongeza lakini mimi nitapongeza kwa jumla nitapongeza sana mabadiliko yanayotokea ni mabadiliko yanayokuja kimaendeleo tunasema tubadilike siku zote na hii ndio *feasibility* ambayo inabebwa na usemi mkubwa sana wa Mapinduzi Daima.

Sasa nikianza mchango wangu sasa naingia kwenye swali la kwanza yaani agizo la kwanza namba moja ambalo liko kwenye ibara ya pili agizo limesema kamati imetaka Serikali kupitia Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kuongeza bajeti kwa ajili ya Tume ya Kitaifa ya Uratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya imendelea ni kwamba hili ni agizo kwa kweli ni zuri sana tunaona juhudi kubwa sana zinazo chukuliwa katika kupambana na madawa ya kulevya kwa kweli juhudi zimekuwa tuseme mara dufu zaidi kuliko vile zilivyokuwa siku za nyuma.

Sasa hapa nikiangalia bajeti imeongezwa kwa asilimia 36 wakati shughuli yenyewe ukweli inaendeshwa kwa kasi ambayo pengine itazidi hata mara 200 zaidi kuliko na hii sasa nasema hii bajeti ni ndogo sana kwasababu madawa ya kulevya ni janga tena ni janga kweli kweli hawa wezi wakubwa wakubwa wasioogopa chochote ni hao wanaotumia madawa ya kulevya, hawa wanaopiga watu mapanga bure bure bila ya sababu ni hao wanaotumia madawa ya kulevya wanaoleta majanga mbali mbali ni hao wanaotumia madawa ya kulevya kwa hivyo kwa sababu ya kupanda kwa shughuli hizi au kuongezeka kwa shughuli hizi basi naona hii bajeti ongezeko na milioni 159,000,000 ni dogo sana sana liangaliwe upya.

Kuna vijana wanatumia dawa hii ya kuzuwiya wasiendelee kulewa naona dawa ile kwa kweli haiwasaidii sana kuwacha madawa kwasababu vile wanavyoipenda saa 6:00 usiku utakuta wamepanga foleni pale wanasubiri dawa ili watumie, sasa wanapotumia dawa ile wanalewa zaidi kuliko hizo dawa za kulevya nashauri hebu iangaliwe ile dawa kweli ina manufaa kwa nini wale wanaipenda sana maana wana *save* kununua madawa na kuona ile kama dawa za kulevya kwa hivyo tuiangalie ile dawa wanayopewa pale Kidogochekundu tuone kama ina faida kubwa au vipi, au tutafute njia nyengine za kuwafanya wasile madawa haya badala ya kuwapa madawa yanayo nanihii zaidi.

Nikiingia kwenye ukurasa huo kuna kifungu cha utekelezaji tena kinapewa hapa kwenye suala agizo la pili kinasema kwamba katika suala la mapambo dhidi ya usambazaji wa matumizi ya

dawa za kulevya Serikali itaendelea kuchukua hatua zote zinazostahiki kama zilivyoelezwa katika sheria zinazosimamia masuala ya dawa ya kulevya.

Miye kwenye sheria ya udhibiti wa dawa ya kulevya ya Zanzibar namba 9 ya 2009 sheria hii imekuwa ikifanyiwa marekebisho sasa haya marekebisho mimi nauliza tu hapa marekebisho yaliyofanya yamefanywa mara ngapi tangu mwaka huu tangu ilipoanza shughuli ya mapambano kwa sura mpya ya madawa ya kulevya.

Halafu ikaendelea pia kwamba kumefanyika marebisho sheria namba 49 haya marekebisho mafanikio yake ningependa tuyajue ili tuone kama tunapiga hatua ya kupingana na madawa ya kulevya.

Nikiendelea tena mbele huko kunasema kwamba sheria zinakidhi haja zilizoko sasa hivi sasa mimi nauliza kama sheria hii inakidhi haja kuna tatizo gani la taasisi hizi zinazohusika na kushughulikia kudhibiti dawa za kulevya kutokushughulikia hili suala kwasababu hapa imesema kwamba sheria inakidhi haja isipokuwa tuu hivi vyombo vinavyoshughulika kwamba labda havikufanya kazi zake kama ipasavyo kwa kui e*valuate* haraka hapa hapa, sasa nasema kama sheria inakidhi haja sasa hawa wanaohusika na kudhibiti wana tatizo gani tena sheria inawaaruhusu chukuweni hatua fanyeni hivi ni rahisi na hapa pia kidogo panataka maelezo ya kina.

Halafu nikiendelea ni Ijumaa leo sitaki kwenda sana nitajitahidi kwenda kwa haraka kuna na agizo namba nne jibu lake hapa nalo linasema kwamba sehemu inasema kwamba miongoni kwa Idara za Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya ni Idara ya Kinga, Tiba, Elimu na Marekebisho na Tabia moja ya majukumu ya idara hii ni kutoa elimu juu ya kinga, tiba na kadhalika na kadhalika sasa miye nasema haya kuna *Sober House* ambazo ndizo zinazoshughulikia.

Hizi *Sober House* ni nyumba za kawaida sana wenzetu India katika kuyashughulia mambo kama haya si India tuu hata Marekani hata Uingereza pengine hata kwengine huko wenzetu wanashughulia hizi kwa vituo maalum ambazo zimejenga kisasa wanaziita sehemu *Healing Centre* na kama wanachukua mpaka waathirika kutoka nje au watu ambao wamepata *stress* kutoka nje wanaweza wakaja kwenye *Healing Centre* wakafanyiwa matibabu ambayo watayafanya tabia zao zielekee kule kunakotakiwa.

Sasa nashauri hapa na sisi tuwe na kama *International* au *National Healing Centre* ambayo itakuwa ni *modify* itakuwa ni bora zaidi kuliko hizi nyumba zetu wanazozifanya *Sober House* nyumba za kawaida.

Halafu jengine agizo namba sita kamati imeshauri kuimarisha kwa mazingira ya upekuaji kwa abiria na mzigo inayoingia na kutoka na kupita bandari na viwanja vya ndege. Hapa mimi nasema bandari na viwanja vya ndege sawa hivyo vinajulikana lakini kuna bandari bubu hizi dawa nyingi zinapitia kwenye bandari bubu halafu pia kuna mahoteli bubu pia huko nako huko nako tuu kuna wasiwasi tuu na madawa ya kulevya na nini halafu kuna watu wana maboti hapa yanakwenda *speed* kali kali sana naona kama wanatembea wanafanya nini na hawa pia

inasemekana wanaleta madawa ya kulevya wanaingizi nchini kwa hiyo na haya pia yaaingizwe kwenye uchunguzi uhakikisha kwamba wanafanikiwa kupiga vita madawa haya ya kulevya.

La mwisho maana leo ijumaa rafiki yangu hapa kanidokeza kwamba leo ijumaa usiseme sana kwa hiyo sitosema sana kwa hiyo la mwisho nasema hebu Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais watufafanuliye kuna neno majanga halafu kuna neno maafa ki-*definition* haya ni mambo mawili sasa lipi kubwa lipi ambalo zaidi litashughulikiwa na Serikali na lipi ambalo kidogo wananchi nao wajikaze kaze kidogo, kwasababu hilo si kubwa kuliko hilo jengine.

Halafu jengine nasema kuna maeneo mwenzangu pale Shihata alizungumza kuna maeneo yanafurika wakati inaponyesha mvua kubwa na eneo moja ambalo nanilifahamu mimi liko kwenye Jimbo langu Garagara pale panafurika kila siku maji, sasa hii Wizara ya maafa hii mimi naishauri iyapitie maeneo kama haya yanayopata mafuriko waweze kusaidia kule kutuwama kwa maji kusiweko ili wasipate tabu ya kuwalipa kuwafidia, kuwasaidia kufanya nini Serikali inakula hasara sana mambo haya ni ya kukinga ni vizuri kukinga kuliko kutibu sasa mimi nadhani ipo haya eneo la Garagara pale panajaa maji panatokea mmomonyoko nyumba za watu zinafurika, mavyoo yanafurika hatari moja kwa moja kiafya kwa hiyo nashauri sana Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ilishughulikie kwa kushirikiana na Wizara zinazohusika kuzihami sehemu hizo ili majanga ya mafurukio yasitokee.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti mimi nikushuukru sana kwa utaratibu wako mzuri sana wa kutupa nafasi sisi wajumbe wako kuchangia na hii ni *concept* ya demokrasia nakushukuru sana, ahsante sana kwa mchango wako naunga sana mkono hii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Dkt. Makame na hapa ndio mwisho wa majadala wetu sasa na namwita Mhe. Waziri kuja kujibu hoja za wajumbe, Mhe. Waziri karibu.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi aidha niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa michango yao mizuri yenye hekima nyingi ambayo yanazidi kusaidia katika utekelezaji wa majukumu yetu, kwa ufupi mengi yalikuwa ni ushuri na ushauri ambao ni sahihi niwahidi waheshimiwa wajumbe tutaendelea kuwafanyia kazi ili tufikie lengo lilikosudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kueleza ningeomba niruhusu kwanza niwatambue waheshimiwa wajumbe wa Kamati yetu Kamati ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa ambayo inaongozwa na:

1. Mhe. Omar Seif Abeid
2. Mhe. Panya Ali Abdalla
3. Mhe. Amina Iddi Mabrouk
4. Mhe. Ame Haji Ali
5. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
6. Mhe. Mussa Ali Mussa
7. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuwataja Wajumbe wa Kamati naomba sasa uniruhusu niwataje wachangiaji waliochangia katika taarifa hii.

1. Mhe. Omar Seif Abeid
2. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)
3. Simai Mohammed Said
4. Mhe. Suleiman Makame Ali
5. Mhe. Masoud Abrahman Masoud
6. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis
7. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi

Waliochangia kwa maandishi ni:-

1. Mhe. Mohammed Mgaza Jecha na
2. Mhe. Machano Othman Said

Mhe. Mwenyekiti, nawashukuru wote kwa michango yao mizuri ambayo imeleta tija sana katika maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba nianze na hili la mwisho ambalo Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi alitaka kujua hii maana ya majanga na maana ya maafa. Majanga ni lile tendo lilisobabisha kutokea hayo maafa, maana yake kwanza tunapata janga. Kwa mfano, ikitokea mafuriko yale mafuriko ndio janga lenyewe, sasa ile athari ya mafuriko ndio maafa yaliyotokea. Kwa hiyo, maafa ni mtoto anayezaliwa kutokana na majanga, na kawaida ya majanga yanasababishwa na sababu mbili. Kuna yale ya kimaumbile ambayo Mwenyezi Mungu anayaleta kwa rehema zake na kuna yale ambayo binadamu wenyewe wanayasababisha. Kwa hivyo, kwanza hutokea janga na matokeo yake yakawa maafa ile athari inayotokea ndio maafa yenyewe na ndio maana ikajuulikana hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, waheshimiwa sana sana walizungumzia masuala ya madawa ya kulevya. Madawa ya kulevya Mhe. Mwenyekiti nataka nikubaliane na Waheshimiwa Wajumbe ni tatizo, na sio tatizo jepesi. Ni tatizo ambalo sisi sote kama viongozi na wananchi tunapaswa kwa pamoja kushirikiana katika mapambano. Na nataka niseme na nirudie tena kusema kwamba sheria iliyopo kwa kiasi kikubwa sana inakidhi haja. Jambo la msingi hapa wasimamizi wa sheria wanatakiwa watekeleze wajibu wao. Lakini katika kutekeleza wajibu wao wanahitaji mashirikiano na wananchi. Kwa hivyo, kuna *challenge* nyingi inayotokea katika utaratibu mzima wa kufanya jambo hilo. Moja katika suala kubwa hapa ni utoaji wa taarifa kwa vyombo vinavyohusika katika utekelezaji. Sasa ndugu zetu wa polisi wanafanya wajibu wao lakini bado wanatakiwa wafanye zaidi, sasa kuna mikakati na mipango mipya iliyopangwa ambayo naamini jitihada hizo za operesheni ya kupambana na jambo hili zitakuwa kubwa zaidi ili ziweze kuondoa tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, moja katika kigezo cha wenye dhamana katika polisi kama Mkuu wa Polisi wa Wilaya, wa Mkoa atakaposhindwa kutekeleza operesheni hii kwa ukamilifu wake maana yake ameshindwa kufanya wajibu wake katika utendaji wa kazi na hatua nyengine za kinidhamu zitafuata juu yake. Kwa hiyo, naamini kutokana na utaratibu huo uliowekwa kutawafanya askari polisi na watendaji wote katika suala hili kusimamia kwa karibu zaidi, na kwa sababu tume yenyewe itakuwa inafatilia nyendo na mwenendo mzima katika kuhakikisha kwamba kila

mwenye wajibu anatekeleza wajibu wake. Kwa hiyo, operesheni zetu naamini zitaongezeka kasi, lakini la muhimu ni mashirikiano ya pamoja na yote yule atakayezembea katika operesheni hizi basi hatua zitachukuliwa ili kuondoshwa katika sehemu ambayo anafanyia kazi ili mapambano haya yashike nguvu na suala hili kwa njia moja au nyengine ima lipungue na ikiwezekana kuondoka kabisa katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu masuala ya uchaguzi mimi nitakubaliana kabisa kwamba upo umuhimu wa kutoa elimu zaidi wa kuendelea kuhakikisha kwamba ofisi zetu za Wilaya zinajengwa, tunachukua kila hatua. Na suala la magari tulisema kwamba watu wa Karakana Kuu wanalifanyia kazi ili kuona gari zipi zitaweza kuendelea kufanyiwa matengenezo ili ziweze kufanya kazi na wakati huo kama nilivyosema tayari tumetengewa milioni mia mbili kwa ajili ya kununua gari mpya. Kadiri uwezo wa serikali utakavyowezekana ndivyo tutakavyosaidia na wenzetu wa Tume ya Uchaguzi ili kupata vitendea kazi na kila hatua zitachukuliwa ili kuelimisha wananchi waweze kufahamu suala zima la umuhimu wa tume yenyewe, kazi wanazozifanya tume na wajibu wa tume katika kufanya shughuli za uchaguzi ili kila mmoja aridhike na tume yetu.

Nataka nichukue fursa hii kuipongeza sana sana Tume ya Uchaguzi kwa kazi nzuri inayofanya naamini itaendelea kufanya kazi vizuri. Tena inafanya kazi kwa uwazi, kidemokrasia na ni moja katika tume ya mfano katika ukanda huu wa Afrika Mashariki kwa namna inavyofanya kazi zake. Wameendesha chaguzi zetu kwa umakini mkubwa, kwa usalama kwa amani na utulivu mkubwa. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wajumbe tuendelee kuunga mkono na kuwapa moyo ili waendelee kufanya kazi zao vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye suala zima la maafa maelezo mengi yalikuwa ni ushauri. Kwa hiyo, nataka niseme napokea ushauri huo wa wajumbe na pale ambapo patahitaji kufanyiwa kazi zaidi tutafanya hivyo. Lakini idara hii ni kama taasisi inayoratibu shughuli wapo watendaji wakuu wa mambo hayo hususan vikosi vyetu vya KMKM, Kikosi chetu cha Ukozi na Zimamoto hivi ni vikosi ambavyo siku zote vinakuwa mstari wa mbele katika kutekeleza majukumu yao katika kuhakikisha pale yanapotokea maafa wanasaidia kwa njia moja au nyengine katika uokozi. Na kama nilivyosema serikali imeshafanya uamuzi katika kujenga hivi vituo vya uokozi, hivi karibuni kama mtakumbuka katika ziara ya Rais alipofanya Mkoa wa Kusini pale Mkoani tuliona kituo kile ambacho kimejengwa na KMKM kitakachosaidia shughuli za uokozi. Kwa hiyo, suala la maafa hili kwa serikali ni suala la kitaifa takriban taasisi zote zinahusika moja kwa moja kwenye mapambano haya ya maafa na mawaziri wote ni wajumbe katika kamati ile ya kupambana na maafa. Kwa hiyo, kwa njia moja au nyengine jitihada zitaongezwa kuhakikisha ule ushauri ambao mmeutoa tunaufanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu kujenga nyumba maalum kwa ajili ya wale wanaoathirika na matokeo ya maafa. Waheshimiwa Wajumbe wazo ni zuri lakini lina gharama kubwa katika kutekeleza kwake na hujui utajenga jengo la aina gani na maafa ya aina gani yatatokea kutokana na janga litakalojitokeza. Kwa hiyo, cha msingi ndio maana tunasema tutamia nyumba hizi za umma kutusaidia na pale kutakapokuwa na uhitaji maalum wa kufanya basi tutafanya ujenzi ule ambao utakuwa na mahitaji maalum kwa ajili ya shughuli maalum. Hivi sasa kwa kushirikiana na taasisi hizi zisizokuwa si za kiserikali tuna mpango ndani ya serikali wa kujenga nyumba maalum au kijiji maalum cha hawa ambao mara nyingi wameathirika na jambo hili ili kuwahamisha katika

maeneo yao wapate maeneo yaliyo salama zaidi na wakae hapo na itatazamwa hatua kwa hatua wale walioathirika zaidi ndio watakaopata fursa za mwanzo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia kuna mradi wa *ZUSP* unafanya kazi kubwa katika kutatua tatizo la yale maeneo ambayo yana athari zaidi. Kupitia kamati ya wataalamu iliyoundwa kwa nia ya kutafuta nusura hiyo imefanya kazi kubwa kamati ya wataalamu, imepata tathmini kubwa na imeainisha maeneo ya hatarishi zaidi. Serikali wanayafanyia kazi kwa kiasi kikubwa kuondoa matatizo hayo ikiwemo suala la bwawa la Mwanakwerekwe na lile la Kibonde Mzungu kule na maeneo mengine ambayo yana athari zaidi. Kwa hiyo, nataka niwaambie Waheshimiwa Wajumbe serikali inalielewa jambo hili na inalichukulia kwa uzito wake inategemea sana na uwezo wetu wa kifedha kwa maana ya kibajeti. Lakini kadiri hali itakavyokuwa nzuri tutachukua hatua.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu miradi ya *TASAF* hususan ile *TASAF I* na *TASAF II*. Waheshimiwa hii miradi tayari imeshakabidhiwa kwa taasisi husika lakini sisi kama waratibu tutafanya kila jitihada kuhakikisha tunawakumbusha hizo taasisi husika kuendelea kusimamia miradi hii, kwa sababu fedha nyingi zimetumika miradi hii iwafae wananchi. Kwa hiyo, tutakuwa na kikao maalum na hizo taasisi husika ili tuzungumzie namna ambavyo tutaihuwisha ile miradi kutokana na umuhimu wa kuhudumia wananchi. Kwa hiyo, tutafanya kila jitihada inayowezekana katika kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanaendelea kupata fursa hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, lilikuwepo suala kuhusu wale waliopoteza sifa ni wangapi? Mhe. Mwenyekiti, kutokana na tathmini iliyofanywa kwa upande wa Pemba ni Kaya 292 zimepoteza sifa, kuna wale ambao waliokuwa hawakutimiza sifa, kuna waliolewa, kuna waliohama, kuna waliofariki na kuna waliopata uwezo wa kujitegemea wanapoteza ile sifa na kuondoka katika kuendelea kupata ruzuku. Kwa hivyo, wanapoondoka hawa utaratibu unafanywa ili wale ambao wana sifa waweze kuingia katika utaratibu wa kufanya kupata ruzuku.

Mhe. Mwenyekiti, na kwa upande wa Unguja kwa sababu bado zoezi halijamalizika tumeanza kwa Wilaya ya Magharibi tu nayo imeonekana Kaya 58 zimepoteza sifa, lakini bado tutaendelea na Wilaya nyengine baada ya hapo tutajua kwa ujumla wake. Lakini mpaka sasa Kaya 350 zimepoteza sifa kwa Unguja na Pemba kazi bado inaendelea na tutaendelea kutoa taarifa katika Baraza hili tukufu kwa kadri itakavyoonekana inafaa ili kuwaelimisha na kuwatambulisha Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali suala kubwa hapa ni lilitiliwa mkazo kuhusu kulipwa kwa madeni wanayodai. Jumla ya madeni yote wakala wanadai kwa taasisi mbali mbali za kiserikali ni milioni 364,000,000 lakini kutokana na jitihada ambazo sasa zimefanyika na maelekezo ya serikali nashukuru sana tayari milioni 82,000,000 zimeanza kulipwa kwa wakala. Kwa hiyo, naamini na wale wengine wataendelea kujitahidi kuendelea kulipa madeni yao ili kuiwezesha wakala kufanya kazi zao vizuri. Nia na dhamira ya wakala wa serikali ni kufanya kazi kwa ubora zaidi, kwa wakati na kwa kiwango kinachotakiwa, hizo ndio jitihada zetu. Na suala zima la kuimarisha masoko ili kiwanda kile kiweze kukidhi mahitaji ya wateja wake.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa suala zima la watu wenye ulemavu. Waheshimiwa Wajumbe, jambo hili ni la msingi wenzetu hawa wana mahitaji maalum kwa hiyo tutazidisha kuongeza nguvu, kushirikiana na taasisi hii au idara hii kwa kuhakikisha kwamba tunawasaidia wenzetu ili kujenga uwezo kwa kila itakavyowezekana kuwawezesha kufanya shughuli zao za kujiendeshea maisha hususan pale wanapoanzisha miradi yao midogo midogo. Nataka nimpongeze sana waziri anayesimamia masuala ya uwezeshaji kwa kukubali na kumteua mmoja katika watu wenye ulemavu kuwa mjumbe katika bodi ile ya mikopo ya uwezeshaji, jambo ambalo linajenga nguvu ya kusikiliza mahitaji yao. Tutaendelea kuwa karibu nao ili tutatue matatizo yao.

Mhe. Mwenyekiti, na suala zima la muongozo ambalo litatoa taaswira kwenye masuala ya ujenzi, mambo ya miundombinu ili kuwe na fursa kwa watu wenye ulemavu kutumia vizuri kama vile ambavyo wenzetu wanatumia, ikiwa ni ujenzi basi lazima ujenzi ukidhi pia haja ya watu wenye ulemavu. Tunapojenga barabara vile vile zikidhi haja za watu wenye ulemavu na kadhalika na kadhalika. Hiyo ndio nia ya serikali kwa hivyo muongozo huo utatuongoza taasisi mbali mbali za kiserikali na za kibinafsi zitaelewa.

Waheshimiwa Wajumbe, kwa sababu ya muda naamini nyote kwa kiasi kikubwa mlitupongeza na mimi nachukua shukurani hizo za kutupongeza kwetu na kuwahakikishia kutoa huduma bora kwa wananchi wetu na kushirikiana kufanya kazi pamoja. Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti nashukuru sana na naomba kutoa hoja. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa na Mhe. Waziri nimpongeze kwa majibu yake wale ambao wanakubaliana na ripoti ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, wanaokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Waheshimiwa Wajumbe, kwanza sina budi niwapongeze kwa kazi nzuri ambayo kuwa mmeifanya ya kuweza kuipokea na kuijadili na kuikubali, na hadi hapa ni mwisho wa kikao chetu na nakiahirisha hadi saa 11:00 jioni

Waheshimiwa Wajumbe, samahani naomba radhi naahirisha mpaka siku ya Jumatatu saa 3:00 asubuhi.

(Saa 6:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 02/10/2017 saa 3:00 asubuhi)